SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Shahidi** kesi ya Mbowe augua ghafla, akatiza ushahidi

UKURASA 5



**GUARDIOLA: HAKUNA UBINGWA JANUARI**

UKURASA 22

Nipashe
Jumanne Januari 18, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580829
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Vurugu Machinga

●●● **Polisi** wawatawanya kwa mabomu ya machozi, wenyewe wataka kuendelea...*Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wafanyabiashara wa Soko la Ilala Mchikichini lililoteketea kwa moto wakiwa na mabango yao, wakitaka kujenga mabanda wenyewe ili waendelee na biashara kabla ya kutawanywa na Polisi wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mke wa Sabaya adai askari wenye silaha waliwavamia

UKURASA 3



## Baadhi shule zashindwa udhibiti UVIKO-19

UKURASA 2

**MICHEZO** **MUKOKO AIGOMEA YANGA SC** UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwasili Uwanja wa Ndege wa Abu Dhabi kwa ziara ya kiserikali katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E), (kulia kwa Rais) Balozi wa Jamhuri ya Tanzania U.A.E, Mohammed Mtonga. **PICHA: IKULU**

# Vurugu Machinga, polisi wawatawanya

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi jana limelazimika kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wafanyabiashara wa Soko la Mchikichini, Ilala jijini Dar es Salaam, baada ya kufunga barabara na kuandamana kuelekea ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo.

Soko hilo liliteketea kwa moto usiku wa kuamkia juzi na kusababisha vitu vyote vilivyomo ndani kuungua.

Wafanyabiashara hao, walikuwa wakishinikiza kuruhusiwa kujenga vibanda vya muda na kuendelea na biashara zao wakati wakisubiri uchunguzi kutoka kwa timu iliyoundwa kuchunguza chanzo cha moto huo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao walisema ni vigumu wao kusubiri siku hizo saba za uchunguzi bila kujishughulisha na chochote kwa kuwa wanategemea kuendesha maisha yao kupitia biashara wanazofanya katika eneo hilo.

"Sisi ombi letu ni kwamba serikali ituonee huruma, ituruhusu tuweke vibanda vya muda tuendelee na biashara, kusubiri mpaka siku saba tutaishije na familia zetu zinazotegemea?" Alihoji mmoja wa wafanyabiashara aliyejitambulisha kwa jina moja la Masawe.

Akizungumza baada ya kufika katika eneo hilo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng`wilabuzu Ludigija, alisema makubaliano ambayo wamefikia ni kuwaruhusu waingie katika eneo hilo kuweka alama katika maeneo yao kwa usimamizi wa timu iliyoundwa.

Pia alisema kwenye maeneo yao, watalazimika kutambuana ili kudhibiti mamluki.

"Unajua kunapotokea majanga kama haya, huwa hakukosi mamluki, kwa hiyo makubaliano yetu na wafanyabiashara ni kwamba, watangia kwenye eneo hili kwa makundi kuweka vigingi (alama) kulinda maeneo yao, na kazi hii itaanza sasa (jana).

Kadhalika, alisema baada ya siku saba za uchunguzi na ripoti kutolewa ndipo wataruhusiwa kuanza kujenga vibanda vyao na kuendelea na biashara zao kama kawaida.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa huo wa Dar es Salaam, Makalla, alisema tayari timu iliyoundwa kuchunguza tukio hilo imeanza kazi.

"Niwasihi wafanyabiashara wa eneo hili kuendelea kutoa ushirikiano ili serikali ijue chanzo na mwisho mapendekezo na ushauri."

"Wakati timu inafanya kazi yake katika siku hizi saba, eneo liwe wazi kama ilivyo sasa na baada ya hapo, tutatoa taarifa hiyo na hatima ya nini kinaendelea."

# Shule zashindwa kuzingatia tahadhari dhidi ya UVIKO-19

**Na Jenifer Gilla**

MRUNDIKANO wa wanafunzi kwenye vyumba vya madarasa na kutozingatia tahadhari ya UVIKO-19, umebainika katika baadhi za shule zilizofunguliwa jana jijini Dar es Salaam.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini baadhi ya shule zilizoko Manispaa ya Temeke, Ilala, Ubungo na Kinondoni hazikuwa na vifaa vya kunawa mikono, wanafunzi na walimu kuvaa barakoa na kukaa kwa umbali unaotakiwa kwa mujibu wa mwongozo wa afya wa kujikinga na ugonjwa huo.

Baadhi ya shule za msingi zilionekana wanafunzi wakibanana, huku wazazi wakishukuru watoto wao kupata shule jirani na nyumbani kuepusha usumbufu wa kwenda umbali mrefu, bila kujali wanakaa wangapi kwenye darasa.

Aidha, kwenye baadhi ya madarasa wanafunzi walikuwa zaidi ya kiwango kilichowekwa kwenye darasa moja, huku kwenye dawati moja wakikaa wanne. Katika Shule ya Msingi Vetenari, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, madarasa yalikuwa yamejaza wanafunzi huku wakikaa bila kupeana nafasi.

Katika shule hiyo darasa la kwanza lenye mikondo minne (A-D) kila mkondo ukiwa na zaidi ya idadi ya kiwango kinachotakiwa cha wanafunzi 40 hadi 45 kwa darasa moja.

Walimu walionekana kutozingatia uvaaji wa barakoa na kuachiana nafasi ya umbali wa mita moja tofauti na mwongozo uliotolewa na Wizara ya Afya na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Wakati Shule ya Msingi ya Ruvuma, ikiwa na wanafunzi zaidi ya idadi inayotakiwa, kulikuwa na ndoo moja pekee ya kunawia mikono na uvaaji wa barakoa haukuzingatiwa.

Hali hiyo ilionyesha kuwatia hofu baadhi ya wazazi waliokutwa nje ya shule hizo wakisubiri kuwachukua watoto wao.

"Yaani na janga hili la corona linaloendelea natamani dawati moja wakae watoto wawili ili kupunguza maambukizi, lakini sasa tutafanyaje wacha wasome tu Mungu atasaidia," alisema Radhia Abdallah.

"Kwa hali hii tuendelee kuomba Mungu hii Omicron (kirusi kipya) isisambae nchini maana watoto wetu hawatopona na ndiyo watatuletea majumbani," alalamika, Anastazia mzazi mwenye mtoto katika shule hiyo.

Katika Shule ya Msingi Ruvuma, Nipashe ilikuta mwalimu wa darasa la kwanza akiwa amezongwa na kundi la watoto kila mmoja akitaka kusahihishiwa daftari lake hali ambayo inahatarisha maambukizi ya kirusi hicho cha corona.

**ADA ZAFUTWA**

Pamoja na changamoto hiyo, wazazi walioandikisha watoto wao darasa la kwanza walipongeza maboresho sekta ya elimu hasa kwa kutodaiwa fedha yoyote.

Sakina Saidi, aliyeandikisha mtoto wake katika Shule ya Msingi JICA, iliyoko Tabata, Manispaa ya Ilala, alifurahia kutotakiwa kutoa mchango wowote wakati wa mchakato huo zaidi ya kutoa fedha kidogo kwa ajili ya kununua vifaa muhimu vya mtoto vya shule.

"Nimetoa Sh. 27,000 tu ambayo wamenipatia sweta, 't-shirt', lebo pamoja na madaftari, kwa kweli hakukuwa na fedha ya ziada, naishukuru sana serikali," alisema Sakina Saidi.

Wakati wengine walifurahia kutodaiwa hela ya chai kwa mwalimu ili kupata nafasi ya kuandikisha mtoto, kitendo ambacho wanasema kilishamiri miaka ya nyuma.

"Miaka ya nyuma huu mtindo ulishamiri sana, unaambiwa nafasi hakuna, ukibembeleza sana unaambiwa utoe Sh. 15, 000 ya chai ya mwalimu ndiyo upewe nafasi, mwanangu aliyepo darasa la sita aliingia kwa mtindo huo, nashukuru huyu aliyeingia mwaka huu japo nafasi za shida, lakini sikuombwa," alisema. Juhudi za gazeti hili kuwapata wakuu wa wilaya hizo kuzungumzia hali hizo hazikuzaa matunda, na pia simu ziliita bila majibu.

## HABARI KITAIFA



Ofisa Usajili wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Yusuph Mwakasyafuka, akitoa mafunzo kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM) kuhusu huduma zinazotolewa na taasisi hiyo na jinsi ya kuzipata kwa njia ya mtandao. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Jaji Mkuu awafunda Mahakimu Wakazi kutenda haki

**Na Hellen Mwango**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, amewataka Mahakimu Wakazi wapya 29 wa Mahakama za Mwanzo, kuzingatia kanuni na kusimamia haki bila kujali kupokea maelekezo kutoka kwa mtu yeyote akiwamo yeye.

Kadhalika amesema, ikitokea Jaji Mkuu akapiga simu kuelekeza jinsi ya kutoa hukumu ya kesi fulani, haraka hakimu mhusika akatoe taarifa Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Jaji Mkuu alitoa rai hiyo jana katika Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki, jijini Dar es Salaam, wakati akiwaapisha mahakimu hao.

"Kazi ya Mahakimu na sisi majaji ni kufanyakazi kwa kuzingatia kanuni zetu, ikitokea hakimu unapigiwa simu na Jaji Mkuu akikuelekeza utoaji wa hukumu kesi unayoisikiliza, mara moja katoe taarifa Tume ya Utumishi wa Mahakama," alisisitiza Jaji Mkuu.

Akifafanua zaidi alisema misingi ya mahakimu ni kutenda haki kupitia ngazi mbalimbali, wakikosea wanakosea mfumo mzima wa utoaji haki.

"Ninyi ni matunda ya wazazi wenu na hazina ya taifa letu, miaka 25 ijayo mtashika nyadhifa mbalimbali za uongozi wa Mahakama Tanzania, lazima muelewe sheria na taratibu za utoaji haki," alisema Jaji Mkuu.

Aidha, alisema mahakimu na majaji wanamamlaka ya mwisho katika utoaji haki ambayo huanzia ngazi ya polisi pale mwananchi anapokwenda kutoa taarifa, upelelezi, kwa waendesha mashtaka Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama ya Rufani.

Naye Jaji Kiongozi, Mustapha Siyani, aliwataka wakatende haki kwa kufuata sheria na taratibu za mahakama kwa kuwa ni mhimili unaoaminika na kuwasihi wasiutie doa kwa vitendo vya rushwa.

Alisema kwa ukubwa na thamani ya kazi waliyopewa na taifa, waende wakachape kazi kwa juhudi na uadilifu na wakaijenge mahakama kwa kusimamia haki.

# Baba adaiwa kubaka wanawe 3 wa kuwazaa

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imeeleza kusikitishwa na tukio la baba Jackson Naiko (57), kudaiwa kuwabaka watoto wake watatu wenye umri wa miaka 15, 17, 18 kwa nyakati tofauti. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini katika wizara hiyo, Prudence Constantine, katika kijiji cha Ndaleta wilayani Kiteto, mkoani Manyara, mtuhumiwa alishakamatwa na yupo mikononi mwa polisi kwa taratibu zaidi za kisheria.

Kadhalika, watoto hao wameshapatiwa huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii.

"Kutokana na kuongezeka kwenye jamii matukio ya ukatili, wizara inawaomba wananchi kutoa taarifa za haraka pale tukio linapotokea au viashiria vyovyote vya ukatili," alisema.

Aliomba viongozi wa dini wakati wa ibada watumie jukwaa hilo, kuendelea kukemea vitendo vya ukatili ili kuleta amani na utulivu kwenye jamii.

"Wizara kwa kushirikiana na wadau wote inaendelea kuimarisha mifumo kwa ajili ya kudhibiti ukatili katika jamii," alisema kwenye taarifa hiyo.ZKutokana na tukio hilo, alisema wizara imewataka wananchi kuungana kupinga ukatili wa makundi yote na kutoa taarifa mapema kwenye vyombo vya serikali na kijamii ili kukomesha matukio hayo.

Taarifa kutoka kijijini humo zinaeleza kuwa baba huyo amekuwa akifanya vitendo hivyo kwa miaka miwili huku akitishia kuwaua watoto hao iwapo watakataa kufanya hivyo na kutoa siri hiyo.

"Baba yao ni mlevi sana na amekuwa akiwafanya hivi watoto wangu akiwa ameshalewa na nikiwa safarini hasa niliposafiri kwenda kumuuguza bibi yangu. Naomba serikali inisaidie," alisema mama wa watoto hao ambaye jina lake limehifadhiwa.

"Tuligundua hili hivi karibuni baada ya usiku mmoja kuona mtoto (binti) akizunguka kwa kutokea alipokuwa analala na kwenda alipokuwa analala baba yao. Tuliweka mtego na muda mfupi ndipo tukasikia mtoto analia, tulipogelea lile eneo baba yao akawa anatutisha kutuchoma kwa kisu huku akisema msinisogelee," alisema mama huyo.

# Mke wa Sabaya adai walivamiwa na kukamatwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKE wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ameieleza mahakama kuwa walivamiwa na kukamatwa na askari polisi waliokuwa wamevalia nguo za kiraia wakiwa wamebeba silaha.

Jesca Thomas (28), ambaye ni shahidi wa pili wa utetezi, kwenye kesi ya uhujumu uchumi namba 27, alitoa ushahidi wake jana mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Alidai simu iliyodaiwa mahakamani ni ya Sabaya na kuonekana kuwapo jijini Arusha, Januari 22, mwaka 2021 ni ya kwake, lakini usajili wa laini ulikuwa kwa jina la Mkuu huyo wa zamani wa Wilaya ya Hai.

Katika kesi hiyo mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akiongozwa na wakili wa upande wa utetezi, alidai kwamba ni mkazi wa Sakina jijini Arusha na anajishughulisha na kazi za kilimo, ufugaji na biashara ndogo.

Shahidi huyo alidai mahakamani kwamba anamfahamu Ole Sabaya kwa kuwa ni mume wake.

"Nina mfahamu tangu 2016 na amekuwa mume wangu tangu 2018," alidai.

Alidai kwamba Januari 22, 2021, alikuwa Bomang'ombe, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro asubuhi alikuwa akifanya shughuli zake za kawaida na majira ya mchana alikwenda mkoani Arusha.

Pia, alidai mahakamani hapo kuwa siku hiyo majira ya asubuhi akiwa nyumbani, Sabaya alimweleza kuwa anakwenda ofisini kwake kwa kuwa alikuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Hai.

Shahidi huyo alidai kwamba kwa kuwa siku hiyo ilikuwa ya Ijumaa alikwenda mikoani Arusha, eneo la Kisongo kwa kuwa ni sehemu anayofanyia biashara zake na alipigiwa simu na mteja kumjulisha kuwa alikuwa anahitaji bidhaa ya mahargwe.

Alidai siku hiyo akiwa nyumbani, Sabaya alichukuliwa na gari la serikali likiwa na dereva wa serikali na alimpeleka ofisini.

Aidha, alidai namba ya simu ya mkononi iliyodaiwa mahakamani kwamba ni ya Sabaya sio yake, bali alisajili kwa jina lake na wamekuwa wakitumia pamoja kwa ajili kufanya mazungumzo yao binafsi.

Alidai kwamba Mei 27, mwaka 2021, alikuwa jijini Dar es Salaam majira ya usiku wakiwa na Sabaya, walisikia watu wakigonga mlango na baadaye kufungua mlango na kuwavamia.

Alidai, baada ya kuingia ndani Sabaya aliwauliza kuwa ni kina nani na walijitambulisha ni askari polisi.

"Walituambia tukae sehemu moja na walifanya upekuzi baada ya kumaliza walituambia wanaondoka na sisi kuelekea Ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)," alidai shahidi huyo.

Wakati wakipekuliwa na askari hao majira saa 10 usiku, alidai kuwa hawakupewa nyaraka yoyote kabla ya kufanya upekuzi huo.

"Walikuwa ni askari polisi kwa kuwa walikuwa na mitutu ya bunduki na hawakutufahamisha chochote wala kutupa nyaraka yoyote ya kuwatambulisha na walitukuta tukiwa wawili chumbani," alidai.

Askari hao alidai, waliondoka nao wawili kuelekea katika ofisi za TAKUKURU makao makuu yaliyopo Upanga, Dar es Salaam.

"Tulipofika tuliandikisha vitu walivyotukuta navyo vikiwamo simu, fedha na gari na baada ya hapo walituambia tusubiri," alidai.

Juni 3, mwaka 2021, alidai walikuwa jijini Dar es Salaam na baada ya kukamatwa walisafirishwa kupelekwa Arusha, akiwa mmojawapo, Sabaya na washtakiwa wengine.

"Tulipofika ofisi za TAKUKURU tulishushwa kwenye gari na kuingizwa kwenye vyumba kwa ajili ya kila mmoja kuhojiwa," alidai shahidi huyo.

Pia alidai kwamba Januari 22, Sabaya alikuwa ofisini kwake Wilaya ya Hai na Januari 23 mwaka 2021, alikwenda kusali kanisani kwa kuwa ilikuwa siku ya Jumamosi ya Sabato.


Boston Auction

3016, Dar es salaam
Mikumi Street, Magomeni
Kinondoni - Tanzania

**NOTISI / TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**Boston Auction Mart & General Agency Co. Ltd P.O. BOX 3016 MWANZA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **LETSHEGO BANK (T), S.L.P.11142 - MWANZA,** TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) TOKA TAREHE TAJWA KWENYE TANGAZO HILI KWA WADAIWA WAFUATAO WALIPE MADENI YAO WANAYODAIWA KWA MUDA MREFU. ENDAPO WATASHINDWA KULIPA KWA MUDA HUO DHAMANA ZAO ZITAUZWA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA KAMA ZILIVYO ORODHESHWA;

| NO | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI/ MMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA / SIFA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 01. | SELEMANI L.MAGUHA | ROBERT CHRISTOPHER MASAHI | NYUMBA ZILIZOPO KIWANJA NO.1063 & 1061 HATI NO. 78454 & 652898 BLOCK "M" PASIANSI MWANZA | 31/01/2022-JUMA TATU KUANZIA SAA 6:30 ALASIRI NA KUENDELEA |
| 02. | RODAN SECONDARY SCHOOL | DANIEL O.KITEGWA & DORCA JACOB | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NO.376 HATI NO.57034 BLOCK "A" KASHISHI NYAMHONGOLO -MWANZA | 31/01/2022-JUMA TATU KUANZIA SAA 8:30 MCHANA NA KUENDELEA |
| 03. | ULIMWENGU LUCAS KITUMBU | ULIMWENGU LUCAS KITUMBU | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NO.156 HATI NO. 79003 BLOCK "H" EAST NYASAKA - MWANZA | 02/01/2020-JUMATANO KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 04 | SELEMANI MAGUHA | JACKSON ROBERT KABALA | NYUMBA ZILIZOPO KIWANJA NO.377 HATI NO.28047 BLOCK "A "MKOLANI MWANZA | 02/01/2020-JUMATANO KUANZIA SAA 8:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| 05 | YUSTHER YONA NGASSA | YUSTHER YONA NGASSA | KADI YA GARI T 537 BAL | |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO BAADA YA NYUNDO YA DALALI KUTUA NA SALIO LA 75% LIWE LIMELIPWA NDANI YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA.
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**PIGA SIMU NO. 0786 600 606 / 0759 707 153/0658 707 153**
**AU**
**KUPITIA LETSHEGO BANK, PIGA SIMU NO. 0658 999 154**

***WOTE MNAKARIBISHWA.***

# Matokeo mabaya kidato cha nne yasababisha atake kujiua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWANAFUNZI mwenye umri wa miaka 17 (jina linahifadhiwa), amenusurika kifo kwa kunywa mafuta ya taa baada ya kupata matokeo mabaya ya kidato cha nne.

Mwanafunzi huyo, alikunywa mafuta hayo Januari 15, mwaka huu, baada ya Baraza la Mitihani kutangaza matokeo hayo.

Akizungumza na gazeti hili, mwanafunzi huyo alisema hakutegemea kupata matokeo hayo kwa kuwa hii ni mara ya pili kufanya mtihani huo.

"Mara ya kwanza nilifanya mtihani mwaka jana nimepata daraja la nne la ufaulu na mara hii nimepata alama C ya Kiswahili matokeo ambayo sikuyategemea, ghafla nimejikuta nimekunywa mafuta wala sikutegemea kwa sababu nilikuwa na msongo wa mawazo," alisema.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu tukio hilo, Kamishna wa Polisi na Kamanda Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Abdallah Hussein Mussa, alisema mwanafunzi huyo baada ya kunywa mafuta aliishiwa nguvu na kupoteza fahamu.

Hata hivyo, Kamanda alisema, alikimbizwa Hospitali ya Mnazimmoja kwa ajili kupata matibabu.

"Ameamua kuchukua maamuzi ya kutaka kujiua baada ya kupata matokeo mabaya katika mitihani yake ya kidato cha nne," alisema.

Alisema tukio lolote la kutaka kujiua ni kosa kinyume na sheria, na kwamba Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi na utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

Aliwataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao ili kujua changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi.

Katibu wa Hospitali ya Mnazimmoja, Hassan Makame Mcha, alisema walimpokea majeruhi huyo Januari 15, majira ya usiku.

Alisema alifikishwa hospitalini hapo akiwa hana fahamu kutokana na kunywa kiwango kikubwa cha mafuta ya taa.

"Baada ya kupatiwa matibabu alipata nafuu na tayari ameshapata ruhusu kurejea nyumbani kwao," alisema.

Kwa upande wake mama mzazi wa mtoto huyo, ambaye hakutaka kutajwa jina lake litajwe gazetini, alisema wakati tukio hilo linatokea alikuwa kazini na alipewa taarifa kutoka kwa majirani.

"Tukio hili limenisikitisha sana na wala sikutegemea, lakini nashukuru Mungu anaendelea vizuri," alisema.

Mtaalamu wa ushauri nasaha, Asya Saleh, alisema elimu ya ushauri nasaha inahitajika kwa wanafunzi shuleni, ili wanapokuwa na msongo wa mawazo waepuke kuchukua uamuzi mgumu.

## Waandishi ajali ya Mwanza watoka ICU

**Na Christina Mwakangale**

WAANDISHI wa habari wawili waliojeruhiwa kwenye ajali ya gari mkoani Mwanza, Tunu Heman na Vanny Charles, wameondolewa kwenye chumba cha uangalizi maalumu (ICU).

Mwenyekiti wa Mwanza Press Club, Edwin Soko, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe jana na kwamba wanaendelea kupatiwa matibabu Hospitali ya Rufani Bugando.

Alisema hali za waandishi hao zinaimarika kutokana na mazungumzo kati yake na madaktari akisema, Vanny anaandaliwa kiti mwendo cha baiskeli ambacho kitamsaidia kuinuka kitandani, badala ya kulala muda mrefu.

"Wanaendelea vizuri hali zao zinaimarika. Wamehamishiwa kwenye wodi pamoja na wagonjwa wengine kutoka katika uangalizi maalumu. Vanny anasumbuliwa na uti wa mgongo pia Tunu alipata maumivu ya shingo na jeraha kwenye nyonga. Wamelazwa Hospitali ya Rufani Bugando.

"Juzi, nilizungumza na madaktari bingwa wakasema majeraha yao hayana haja ya upasuaji wanahitaji mazoezi zaidi. Wataanza mazoezi labda kuanzia leo (jana) kwa kutumia wheel chair," alisema Soko.

Kadhalika, Soko alisema umoja huo wa wanahabari Mwanza, unaushukuru uongozi wa mkoa pamoja na Hospitali ya Bugando na wadau wengine kwa kutoa ushirikiano na kuendelea kuwapatia huduma wagonjwa hao.

"Gharama zinachangiwa na mkoa na Bugando ni wadau wetu, hata vifaa hakuna changamoto."

Baada ya ajali, Kamanda wa Polisi mkoani Simiyu, ACP Blacius Chatanda, alisema mwandishi wa habari Vanny na Tunu, walikimbizwa hospitali ya rufani ya Kanda ya Ziwa kwa ajili ya matibabu.

Ajali hiyo ilisababisha vifo vya waandishi wa habari watano, akiwamo Husna Mlanzi (ITV), Johari Shani (Uhuru Digital), Antony Chuwa (Habari Leo Digital), Abel Ngapemba, Ofisa Habari Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mwanza na Steven Msengi, ambaye alikuwa Ofisa Habari Ukerewe.

Kwa mujibu wa kamanda, uchunguzi wa awali ulibaini chanzo cha ajali ni mwendokasi wa magari yote mawili.




Mkuu wa Idara ya Huduma za Kidigitali na Mtandao Vodacom Tanzania, Yvonne Bayona (kulia), akizungumza kwenye kongamano la kidigitali lililofanyika kuhusu mageuzi ya kidijitali kwenye sekta ya kilimo yanavyowezesha jamii kujikwamua kiuchumi. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Quince wood, Fatma Fernandes. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaridhishwa uandikishaji, wanaoanza kidato cha kwanza

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKATI jana shule za msingi na sekondari zikifunguliwa, serikali imeeleza kuridhishwa na uandikishaji na kuripoti kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza katika mwaka huu wa masomo.

Vile vile, imesisitiza kuanza mchakato wa kuajiri walimu na kuongeza matundu ya vyoo katika shule za umma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, aliyasema hayo jana jijini hapo wakati wa ziara ya kutembelea shule wilayani Chamwino kwa lengo la kujionea wanafunzi walioripoti.

Alisema baada ya serikali kukamilisha madarasa kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeanza mazungumzo na Wizara ya Utumishi kwa ajili ya kuajiri walimu na ujenzi wa matundu ya vyoo.

Aliwaagiza wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na maofisa elimu wa ngazi zote, kusimamia kazi iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha wanafunzi waliofaulu wanaripoti na wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa na kusimamia miundombinu hiyo.

"Rais Samia amehakikisha kunakuwa na mahali pazuri pa kusomea kama hapa Shule ya Sekondari Chamwino, nielekeze wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi, maofisa elimu ngazi zote wahakikishe wanafunzi waliofaulu wanaripoti shuleni na wale wenye umri wa kuanza shule waandikishwe," alisema.

Bashungwa aliziagiza halmashauri kutumia sehemu ya mapato ya ndani kujenga nyumba za walimu na kupunguza sehemu ya fedha kutoka Serikali Kuu kuelekeza katika ujenzi wa nyumba hizo lengo likiwa ni kuweka mazingira mazuri.

"Si hivyo tu, pia Rais Samia anawajali walimu wake, hivyo tumejipanga kuhakikisha tunalinda na kutetea maslahi ya walimu ikiwamo kupandishwa madaraja," alisema.

Pia Bashungwa alimwagiza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, shule zote zisizo na hati na mpya maeneo yake yanapimwa na kuwa nazo.

Naye Katibu Tawala Wilaya ya Chamwino, Neema Nyerege, alisema Wilaya ya Chamwino ilipokea Sh. bilioni 2.9 kwa ajili ya kujenga madarasa 146 ya sekondari na vituo shikizi.

**HABARI KITAIFA**

## KESI YA MBOWE

# Shahidi akatisha kutoa ushahidi, akilalamika kichwa kuuma

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa 10, Inspekta Innocent Ndowo, amedai alipewa kazi ya kuchunguza simu nane zikiwamo za washtakiwa katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu na kupata majibu chanya kwenye simu nne.

Hata hivyo, Inspekta Ndowo hakumaliza kutoa ushahidi wake baada ya kudai kichwa kinamgonga sana hayuko katika nafasi ya kuendelea, kadri alivyoendelea kutoa ushahidi kiliuma hadi kushindwa kuzungumza kwa sauti.

Shahidi huyo, alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga, kwa kuongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar.

Alidai alikuwa mapokezi katika kitengo chake cha kazi cha Maabara ya Uchunguzi wa Kisayansi na kupokea kazi kutoka kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI).

Alidai ilikuwa barua na simu nane, tecno nne, Itel mbili, Samsung moja na bundi moja na kisha aliandika barua kuomba taarifa za simu hizo kwa watoa huduma za simu Julai mosi, mwaka 2021 kwa kutumia namba ya kesi CD/IR/2027/2020 ili kuonyesha kuna jinai.

"Majibu nilipata Julai 2, mwaka 2021, niliomba kupata mawasiliano kupitia mtandao wa kijamii, telegram, Facebook, WhatsApp, ujumbe, miamala ya fedha, taarifa za kupiga na kupigiwa, vielelezo vilikuwa nane dhidi ya namba za simu kadhaa.

"Niliomba usajili wa namba tajwa na taarifa zingine zitakazosaidia katika upelelezi, niliandika barua kwenda Tigo na Airtel," alidai shahidi.

Kadhalika, shahidi huyo alidai simu zilizokuwa na majibu chanya ni nne, aliandaa taarifa zake na kuprinti, alipokamilisha aliweka 'seal' ya plastiki iliyokuwa na majina yake, tarehe na sahihi kisha akaenda kuhifadhi katika locker (sehemu ya kuhifadhi) lake.

Alidai kuwa ripoti hiyo aliikabidhi kwa Inspekta Swila, vielelezo vyote vinane, taarifa ya simu nne na ilichukuliwa Agosti 6, mwaka 2021.

Inspekta Ndowo alidai taarifa za miamala na usajili zote ziligongwa muhuli, taarifa ya Tigo ikiwa na nembo yao na taarifa ya Airtel pia ikiwa na nembo yao na kusainiwa na Gladys Fimbari.

Alidai namba za simu zilizoombwa taarifa zake ni 0784 779944, 0782 237913 na 0787 555200.

Alidai namba 0784 779944 imesajiliwa kwa jina la Freeman Aikaeli Mbowe, ilifanya muamala wa Sh. 80,000 Julai 31, mwaka 2020 kwenda kwenye namba 0782 237913 yenye usajili wa Halfani Bwire.

Shahidi aliendelea kudai kuwa Julai 20, 2020 ulifanyika muamala kutoka 0780900174 kwenda 0787555200 wa Sh. 500,000.

Pia alidai Tigo taarifa ya usajili ya namba 0719 933386 ilisajiliwa kwa jina la Freeman Mbowe na simu zenye matokeo chanya zilikuwa Tecno tatu na Itel moja.

Baada ya kutoa ushahidi huo aliinua mkono na aliporuhusiwa alimweleza jaji kwamba kichwa kinamgonga, anashindwa kuzungumza kwa sauti.

"Nilikuja asubuhi kichwa kikiwa kinanigonga ila kadri muda unavyoendelea kinauma zaidi ndiyo maana unaona sauti iko chini," alidai shahidi hiyo.

Wakili Hillar alidai shahidi hayupo katika nafasi ya kuendelea kutoa ushahidi, waliomba kesi iahirishwe.

Mahakama ilikubali kuahirisha kesi hadi leo kama shahidi atakuwa amepata nafuu ya kuweza kufika mahakamani.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanashtakiwa kwa mashtaka sita ya kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, mwaka 2020 maeneo ya Arusha, Morogoro, Mwanza, Moshi na Dar es Salaam.

## Majeruhi ajali ya treni watoka hospitalini

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC), limesema abiria waliojeruhiwa kwenye ajali ya treni iliyotokea eneo la Mkalamo-Mvave, mkoani Tanga, wameruhusiwa hospitalini huku waliokwama eneo hilo wakikamilisha safari yao.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Shirika hilo, Jamila Mbarouk, aliyasema hayo jana akizungumza na Nipashe.

"Majeruhi wameruhusiwa kutoka hospitalini na abiria waliokwama wameshafika Dar es Salaam," alisema Jamila.

Kwenye taarifa yake juzi, Jamila alisema sababu ya ajali hiyo ni mabehewa matano kupinduka na mengine manne kuacha njia.

"Treni hiyo iliondoka Arusha saa 8:30 mchana siku ya Jumamosi, kuelekea Dar es Salaam ikiwa na behewa 14 zilizobeba abiria 700, ilipofika eneo lililoko kati ya Mkalamo na Mvave (km 88) behewa tano na kusababisha majeruhi watano, wanaume watatu, wanawake wawili na kifo cha mtoto," alisema Jamila kwenye taarifa hiyo.

Kadhalika, ajali hiyo ilisababisha kifo cha mtoto Hassan Lugano pamoja na majeruhi watano.

Pia alitaja mabehewa yaliyopinduka kuwa ni namba 3614, 3527, 3605, 3526 na 3530 na zilizoacha njia ni zenye nambari 3662, 3666, 4536 pamoja na behewa la huduma ya chakula na vinywaji 'buffet'.

Jamila, alibainisha kwamba shirika linaendelea kufuatilia kwa karibu kufahamu chanzo cha ajali, ili kuchukua hatua, huku likitoa pole kwa familia ya marehemu na kuwaombea majeruhi wa ajali kupata nafuu mapema na kuendelea na majukumu yao ya kujenga taifa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Safia Jongo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, akisema kifo ni kimoja cha mtoto pamoja na majeruhi watano.

A PRODUCT OF The Coca-Cola Company

KILIMANJARO DRINKING WATER

TAARIFA KWA UMMA

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.




@kilimanjaro_drinking_water kilimanjarodrinkingwater kdw@bbl.co.tz

+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ripoti uchunguzi matukio ya moto zitolewe mapema

**JUZI** soko maarufu la mitumba na bidhaa nyingine la Karume, Mchikichini, Ilala jijini Dar es Salaam, liliungua moto na mali zote kuteketea na kuwaacha wafanyabiashara katika simanzi na vilio.

Tukio hilo linatokea miezi kadhaa ikiwa wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo na Mwenge, hawajasahau machungu waliyokutana nayo kutokana na kuunga kwa masoko hayo.

Moto huo umeteketeza mali nyingi na kuwaacha wafanyabiashara hao watupu, walitoka hatua ya juu kurudi chini huku wenye mikopo wakibaki njiapanda.

Baada ya kuungua kwa Soko la Kariakoo, iliundwa timu ya uchunguzi ambayo hadi sasa haijatoa matokeo, huku kukiwa na mipango ya kuboresha zaidi kwa siku zijazo.

Maeneo haya yote yamewaumiza wafanyabiashara wadogo ambao wameuanza mwaka kwa majonzi kwa kupotelewa na mali zao zote na sasa wanashindwa kurudi kwenye maeneo husika kuendelea na biashara.

Wengi walionekana kukaa chini huku wasijue la kufanya, wakilia vilio vya uchungu na baadhi wakitaka kupenya kwenye moto ili kuokoa chochote, lakini walishindwa.

Kwa ujumla janga hili na mengine yameharibu mwelekeo wa maisha ya wengi, wapo ambao mtaji mzima umeteketea, wamepoteza kila kitu na sasa hawajui waanzie wapi na watatoa wapi mtaji.

Wapo waliokopa kwenye taasisi za fedha wanatakiwa kurejesha fedha, au wapo kutokana na biashara hiyo wanasomesha watoto wao, wanalipa kodi za nyumba na kupata mahitaji yote ya msingi, lakini kwa hali ilivyosasa maisha yao yamesimama.

Tayari imeundwa timu ya kuchunguza tukio hilo na wafanyabiashara wamekatazwa kurudi kwenye eneo hilo, na jana palitokea mvutano baina yao na polisi kwa kuwa walitaka kurudi kujenga vibanda vingine kuendelea na biashara ya kutafuta riziki ya siku.

Timu hiyo inayojumuisha Ofisi Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, Jeshi la Polisi, Kikosi cha Uokoaji na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Aidha, wafanyabiashara hao walipinga uchunguzi kuchukua siku 14, wakidai ni nyingi kwa kuwa wanataka kuendelea kutafuta riziki kwenye eneo hilo.

Tunapongeza hatua za awali zilizochukuliwa na serikali, lakini ni muhimu wakavaa viatu vya wafanyabiashara hao kuona namna ya kuwawezesha kuendelea na biashara zao kuliko mamia ya watu kurudi nyumbani bila kuzalisha kwa muda mrefu.

Maswali ni mengi juu ya chanzo cha moto kwenye masoko haya, matokeo ya uchunguzi unaofanyika, jitihada za kukabili majanga ya moto hata kwenye maeneo ya miji ambayo kuna miundombinu mizuri.

Ni muhimu wafanyabiashara hawa wakasaidiwa kwa kuwa wanatafuta riziki, wanachangia kwenye uchumi wa nchi, wasiachwe hewani bila kujua mwelekeo kama tulivyoona kwenye masoko mengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Zitafutwe mbinu wanafunzi wasiogope, wasifeli Hisabati

Na Sabato Kasika

**MATOKEO** ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2021/2022, yametangazwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), huku Katibu Mtendaji, Dk. Charles Msonde, akisema, watahiniwa hawakufanya vizuri kwenye somo la Hisabati.

Katibu Mtendaji anasema, ufaulu wa somo hilo upo chini ya wastani ya asilimia 19, na kwamba mwaka jana ulikuwa chini ya wastani kwa watahiniwa kupata asilimia 20.12, hivyo, kwa kauli yake, ni wazi kwamba, kuna haja ya kuchukua hatua za kuimarisha kujifunza na kufundisha hesabu ili kusaidia wanafunzi kumudu vyema somo hilo na kuondoa dhana iliyozoeleka miongoni mwao kuwa hesabu ni ngumu.

Ni vyema wanafunzi wakaondolewa fikra hizo, wasiwe wavivu wa kujifunza hisabati, lakini kuwe na hamasa kutoka kwa walimu ya kuhamasisha watoto shuleni kuliona somo hilo kama la kawaida kuliko kulikimbia na kulichukia.

Pamoja na hayo, bado kuna haja ya kuangalia mfumo wa elimu, kwa kuondoa utaratibu wa mtihani wa hisabati kuwa wa kuchagua, kwani unaweza kuwa unachangia wanafunzi kufanya vibaya katika somo hilo. Hebu fikiria, katika shule ya msingi, mwanafunzi anapewa mtihani wenye kuchagua majibu, kwa mazingira kama hayo, ni vigumu kufanya vizuri katika somo hilo, kwani huko anakotokana hakuna utaratibu huo.

Akiwa sekondari, itambidi aumize kichwa kufanya mtihani wa somo hilo, wakati awali alikuwa anachagua majibu, jambo ambalo ni vigumu mwanafunzi kuwa na msingi mzuri wa hisabati.

Ninaamini kwamba, somo hilo linamfanya mwanafunzi atafute mbinu za kupata jibu hasa kwa kuzingatia kanuni, lakini anapoelekezwa kuchagua majibu, hawezi kuwa na msingi imara wa kukokotoa na kupata majibu.

Hivyo, ingekuwa vyema iwapo mfumo wa ufundishaji wa somo hilo, hasa katika shule za msingi utaendelea kama ulivyo na hata kwenye mtihani, wanafunzi watumie waumize vichwa kupata majibu badala ya kuchagua.

Yawezekana mfumo wa kazi, swali, jibu umepitwa na wakati, lakini huenda, ulisaidia wanafunzi kumudu somo hilo, kwani sehemu ya kazi ndiyo inayoonyesha jinsi gani amefanya hadi akapata jibu.

Kwenye suala la mtihani wa hisabati kufanyika kwa kuchagua majibu, wanasiasa wamekuwa wakilaumiwa kuwa wameingilia na kusababisha wanafunzi kutoumiza vichwa kufanya somo hilo.

Kama hilo lina ukweli ndani yake, basi ingependekeza siasa zingeachwa pembeni, ili elimu ichukue nafasi yake hatimaye wanafunzi waweze kumudu somo hilo ambalo ni miongoni mwa masomo muhimu. Vilevile, kuna suala la uhaba wa walimu wa somo hilo, katika shule mbalimbali, jambo ambalo kwa namna moja au nyingine linaweza kuchangia wanafunzi kutofundishwa ipasavyo.

Kwa maana hiyo, ninadhani kuna haja ya uboreshaji wa upatikanaji wa walimu, ili wawe wa kutosha, ambao wameandaliwa vya kutosha wakaiva na wawe na vitendea kazi ili wafanye kazi yao kikamilifu.

Hatua hiyo inaweza kwenda sambamba na kupunguza wingi wa wanafunzi katika darasa moja ili mwalimu awe na unafuu katika ufundishaji, kwani sidhani kwamba, ni rahisi kufundisha wanafunzi 100 kwa wakati mmoja.

Lakini pamoja na hilo, kuna haja ya wanafunzi kupewa majaribio ya mara kwa mara ya somo hilo, waweze kulizoea hata katika mtihani wasipewe maswali ya kuchagua majibu, bali kila mmoja aumize kichwa kupata jibu.

Pamoja na hilo, si vibaya kukawa na motisha kwa walimu wanaofundisha somo hilo, kwani inaweza kuchochea kasi ya kuwafanya wafundishe kwa bidii na kutoa mbinu zitakazofanya wanafunzi walipende.

Kaulimbiu ya walimu na hata wazazi kwa watoto wao ingekuwa ni 'hisabati ni somo rahisi', ili wawe nayo vichwani, walipende, kwani wakiambiwa kuwa ni gumu, ni wazi watafanya vibaya katika mtihani.

# TANGAZO

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## KALAMBO DISTRICT COUNCIL

# THE FINANCIAL STATEMENTS FOR THE KALAMBO DISTRICT COUNCIL FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE 2020

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KALAMBO DISTRICT COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30th JUNE, 2020

| | Notes | 2020 | Restated 2019 |
|---|---|---|---|
| | | TZS '000' | TZS '000' |
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 21 | 1,684,160 | 1,902,771 |
| Receivables and prepayments | 22 | 336,765 | 752,337 |
| Inventories | 23 | 194,766 | 622,969 |
| Non-current assets held for sale | 25 | 34,372 | 40,229 |
| | | 2,250,064 | 3,318,306 |
| **Non-current assets** | | | |
| Property, plant and equipment | 24 | 47,091,387 | 49,195,747 |
| | | 47,091,387 | 49,195,747 |
| TOTAL ASSETS | | 49,341,450 | 52,514,053 |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables | 26 | 695,130 | 1,240,158 |
| Employee benefits | 28 | 2,258,340 | 2,150,368 |
| Deferred income (Grant) | 10 | 414,209 | 1,208,549 |
| Borrowings (Bank Loan) | 27 | - | 12,053 |
| | | 3,367,681 | 4,611,127 |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Deferred income (Grant) | 29 | 1,427,245 | 1,125,360 |
| | | 1,427,245 | 1,125,360 |
| TOTAL LIABILITIES | | 4,794,925 | 5,736,487 |
| NET ASSETS | | 44,546,526 | 46,777,567 |
| Accumulated surplus/(deficit) | | 44,510,526 | 46,741,567 |
| Minimum Compulsory Reserves | | 36,000 | 36,000 |
| TOTAL NET ASSETS | | 44,546,526 | 46,777,567 |

Msongela N. Palela
CMT Chairperson
Date 24/09/2020

Amandus L. Mtani
CMT Secretary
Date 24/09/2020

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KALAMBO

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KALAMBO DISTRICT COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE, 2020

| | Notes | 2020 TZS '000 | 2019 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Local taxes | 8 | 1,107,520 | 811,214 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 9 | 243,540 | 233,455 |
| Amortisation of recurrent grants | 10 | 20,780,989 | 19,189,749 |
| Transfer from other Government entities | 11 | - | 356,413 |
| Revenue from exchange transactions | 12 | 10,726 | 72,555 |
| Amortisation of capital grant | 29 | 1,833,350 | 4,913,653 |
| Other own revenue | 13 | 123,123 | 189,016 |
| | | 24,099,248 | 25,766,056 |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 14 | 18,322,135 | 15,917,619 |
| Supplies and consumables used | 15 | 2,647,056 | 3,840,768 |
| Maintenance expenses | 16 | 504,982 | 486,074 |
| Grants and other transfer payments | 17 | 344,879 | 335,144 |
| Finance costs | 18 | 207 | 17,418 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 24 | 863,581 | 1,265,013 |
| Provision for Impairment of revenue (POS) | 22 | 97,210 | - |
| | | 22,780,049 | 21,862,035 |
| Surplus/(deficit) during the year | | 1,319,199 | 3,904,021 |

Msongela N. Palela
CMT Chairperson
Date 24/09/2020

Amandus L. Mtani
CMT Secretary
Date 24/09/2020

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KALAMBO

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KALAMBO DISTRICT COUNCIL

### STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSETS FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE, 2020

| | Accumulated surplus/deficit | Minimum Compulsory Reserves (MCR) | Total |
|---|---|---|---|
| | TZS '000' | TZS '000' | TZS '000' |
| **At 01 July, 2018** | 43,401,153 | - | 43,401,153 |
| Surplus/(deficit) for the year | 3,904,021 | - | 3,904,021 |
| Adjustment of MCR Reserve**** 1 | (36,000) | 36,000 | - |
| Adjustment of Recognized Inventory | (53,271) | | (53,271) |
| Adjustments of error in PPE****2 | (474,336) | | (474,336) |
| **At 30th June, 2019** | 46,741,567 | 36,000 | 46,777,567 |
| **At 01st July, 2019** | 46,741,567 | 36,000 | 46,777,567 |
| Surplus/(deficit) for the year | 1,319,199 | - | 1,319,199 |
| Property, Plant & Equipment to RUWASA | (3,991,040) | | (3,991,040) |
| Accumulated Depreciation charge to RUWASA | 440,800 | | 440,800 |
| Payable transferred to RUWASA | 334,140 | | 334,140 |
| Receivable Transferred to RUWASA | (334,140) | | (334,140) |
| **At 30th June, 2020** | 44,510,526 | 36,000 | 44,546,526 |

**Disclosure Note ***1:** During the Financial Year the Council was supposed to Contribute TZS 36,000,000 as Minimum Compulsory Reserve to the LGRB however, the Council did not contribute any amount and remained with un-contributed amount of TZS 36,000,000

**Disclosure Note***2:** Adjustment of TZS 474,336,289 relate to amount Inventory which was also accounted in Work in Progress.

Msongela N. Palela
CMT Chairperson
Date 24/09/2020

Amandus L. Mtani
CMT Secretary
Date 24/09/2020

CASH FLOW STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE, 2020
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KALAMBO

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KALAMBO DISTRICT COUNCIL

| | Notes | 2020 TZS '000' | 2019 TZS '000' |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| **Receipts** | | | |
| Taxes and levies | 8A | 966,396 | 892,894 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 9 | 243,540 | 233,455 |
| Recurrent Grants | 10 | 19,868,146 | 20,055,760 |
| Revenue from exchange transactions | 12 | 10,726 | 72,555 |
| Development Grant Received | 41 | 1,784,146 | 4,235,831 |
| Other Own Income | 13 | 123,123 | 189,016 |
| Receipt from 10% contributions to Women & Youth Fund | 21L | 4,156 | - |
| | | 23,000,233 | 25,679,511 |
| **Payments** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 14A | (17,994,891) | (16,140,304) |
| Supplies and consumables used | 15A | (2,533,510) | (3,632,688) |
| Maintenance expenses | 16A | (487,967) | (464,433) |
| Grants and other transfer payments | 17A | (420,620) | (259,403) |
| Contribution to 10% Women & Youth Fund | 39 | (63,200) | - |
| | | (21,500,188) | (20,496,828) |
| Change in Misc. Deposit Account Balance | 21R | 25,529 | 111,539 |
| Transfer to RUWASA | 21 | (195,715) | - |
| Transfer to MOF | 11 | (35,839) | |
| Net cash from operating activities | | 1,385,598 | 5,294,223 |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Acquisition of property, plant, and equipment | 41 | (1,592,156) | (5,059,410) |
| Net cash from investing activities | | (1,592,156) | (5,059,410) |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Cash payments for long term liabilities | 27 | (11,845) | (127,213) |
| Finance costs | 18 | (207) | (17,418) |
| Net cash used in financing activities | | (12,053) | (144,630) |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | (218,611) | 90,183 |
| **Cash and cash equivalents at beginning of period** | 21 | 1,902,771 | 1,812,588 |
| **Cash and cash equivalents at end of the period** | | 1,684,160 | 1,902,771 |

Msongela N. Palela
CMT Chairperson
Date 24/09/2020

Amandus L. Mtani
CMT Secretary
Date 24/09/2020

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KALAMBO

### 1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

Hon. Chairperson of the Council,
Kalambo District Council,
P.O. Box 3,
KALAMBO.

### 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Opinion**

I have audited the Financial Statements of Kalambo District Council, which comprise the Statement of Financial Position as at 30th June, 2020, the Statement of Financial Performance, Statement of Changes in Net Assets, Cash Flow Statement, the Statement of Comparison of Budget and Actual Amounts for the year then ended, as well as the Notes to the Financial Statements, including a Summary of Significant Accounting Policies.

In my opinion, the accompanying Financial Statements present fairly in all material respects, the Financial Position of Kalambo District Council as at 30th June, 2020, and its Financial Performance and its Cash Flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and in the manner required by the Local Government Finances Act, 1982 (Revised 2000).

**Basis for Opinion**

I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the Audit of the Financial Statements section of my report. I am independent of Kalambo District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements and the IESBA Code.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

**Emphasis of Matter**

Without modifying my opinion I draw attention to Note 38 to the Financial Statements which indicates that, Kalambo District Council has pending legal cases filed by two revenue agents of which, preliminary hearings are in progress. The ultimate outcome of the cases cannot presently be determined, and no provision for any liability that may result has been made in the Financial Statements. The initial estimate done by management indicates that, the Council may be obliged to pay a sum of TZS 65,000,000 if the cases will be ruled in favour of the plaintiff.

Contrary to the cited regulation, I noted that, Kalambo District Council received and accepted goods and services worth TZS 130,710,393 without being inspected by the Goods Acceptance and Inspection Committee.

Charles E. Kichere
Controller and Auditor General
Dodoma, United Republic of Tanzania.
31st March, 2021

CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

# Serikali yawagawia pikipiki 300 maofisa ugani Dodoma

**Na Mbaraka Kambona,** DODOMA

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, amekabidhi pikipiki 300 kwa wakuu wa mikoa 25 ili zikatumiwe na maofisa ugani wa sekta ya mifugo waliopo katika halmashauri kwa lengo la kuwarahisishia kazi ya kuwahudumia wafugaji nchini.

Dk. Mpango alikabidhi pikipiki hizo muda mfupi baada ya kufungua kikao kazi cha Washauri wa Mifugo na Wakuu wa Idara za Mifugo na Uvuvi kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa, kinachofanyika kwa siku mbili jijini hapa.

Wakati akikabidhi pikipiki hizo kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Athony Mtaka kwa niaba ya Wakuu wa mikoa wengine, Dk. Mpango alisema sekta ya mifugo ni moja kati ya vipaumbele kwa serikali na ugawaji wa pikipiki hizo kwa maofisa hao ni katika jitihada za serikali kuboresha sekta hiyo ili iweze kuwa na tija kwa taifa.

"Serikali inatambua changamoto za sekta hii napenda kuwahakikishia serikali inaendelea kuzitatua na ndiyo maana leo Rais Samia Suluhu Hassan ameidhinisha kununuliwa kwa pikipiki hizi na tutaendelea kuboresha huduma za ugani ikiwamo kuendelea kutoa elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji wetu," alisema Dk. Mpango.

Aliwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri, Miji na Manispaa kutenga fedha kwa ajili ya kutatua changamoto za maofisa ugani katika maeneo yao huku akiwataka kuzitumia vyema pikipiki hizo ili kuwasaidia wafugaji kufanya ufugaji wenye tija.

Kwa upande wake, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema pamoja na kazi kubwa inayofanyika ya kuboresha sekta ya mifugo, bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya maofisa ugani na kumuomba Makamu wa Rais kuona uwezekano wa serikali kutoa kibali cha ajira.

"Pamoja na uwapo wa teknolojia ya ugani kiganjani, haiondoi uhitaji wa maafisa ugani, uhitaji ni mkubwa, tunaomba serikali iwaajiri maafisa hawa ili waje kusaidia wafugaji wetu huko waliko," alisema Ndaki.

Kuhusu pikipiki hizo, Ndaki alisema serikali imetumia Sh. milioni 864 kuzinunua na zitasambazwa kwa mikoa 25 na halmashauri 140 zinatarajiwa kufaidika.

Naye, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa alisema, ili kuhakikisha sekta ya mifugo inaendelea kuleta tija kwa wafugaji, watahakikisha asilimia 15 inayotakiwa kutengwa na halmashauri kwa ajili ya kuendeleza sekta hiyo, inatengwa na kusimamiwa vizuri zitumike kuendeleza sekta hiyo kama ilivyokusudiwa.

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Tixon Nzunda, alisema lengo la kikao kazi hicho ni kuandaa mikakati ya kuboresha utoaji wa huduma za ugani wa wafugaji ili sekta ya mifugo iweze kuwa na tija zaidi nchini.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (katikati), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, funguo ya mfano ikiwa ni ishara ya kukabidhi pikipiki hizo kwa niaba ya wakuu wa mikoa wengine katika tukio lililofanyika jijini Dodoma. PICHA: **MPIGAPICHA** WETU

## Mbaroni madai kujifanya ofisa wa jeshi

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

MKAZI wa Nyamanoro jijini Mwanza, Abdul Nassoro (49) amependishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora kwa tuhuma za kujifanya ofisa wa Jeshi la Polisi kwa kipindi cha zaidi ya miaka saba.

Mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, Juhudi Mdonya, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Elimajid Kweyamba, alidai kuwa mshtakiwa huyo anakabiliwa na mashtaka mawili.

Akisoma shtaka la kwanza la kukutwa na vitambulisho mbalimbali vya kazi, alidai kuwa Desemba 24, mwaka jana, majira ya saa 7:45 mchana maeneo ya Kituo cha Polisi Kata ya Igunga Mjini, Nassoro alikamatwa na vitambulisho hivyo.

Alidai kwa kipindi cha zaidi ya miaka saba alikuwa akijitambulisha kuwa ni mwajiriwa wa Jeshi la Polisi Tanzania mwenye namba G.3659 CPL Marko.

Kwa mujibu wa Kweyamba, mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 100 (b) kanuni ya adhabu sura ya 16 mapitio ya 2016.

Shtaka la pili ni la wizi wa kuaminika analodaiwa Desemba 8, mwaka jana majira ya saa tisa alasiri katika Mtaa wa Benki mpya, Kata ya Igunga Mjini, aliiba fedha taslimu Sh. milioni 15 ambazo aliaminiwa na kupewa na mtu mmoja aliyetambulika, Kazawadi Bethulabusha, kwa ajili ya kununulia na kumkabidhi kilo 32,000 za mchele, ambazo hata hivyo hakumpatia wala kurudisha fedha.

Kwa mujibu wa Kweyamba mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume na kifungu 273(b) na 265 kanuni ya adhabu sura ya 16 mapitio ya 2019.

Mshtakiwa huyo hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo na alipelekwa mahabusu baada ya kukosa mdhamini mmoja kwa dhamana ya maandishi ya Shilingi milioni tatu.

Kesi hiyo itatajwa tena Januari 28, mwaka huu.

# RC atoa milioni 3 kumjengea mhitaji nyumba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, ameahidi kutoa Shilingi milioni tatu kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa nyumba ya kisasa ya mlengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF), Mwashi Masanja, mkazi wa Itilima, wilayani Kishapu.

Mjema alitoa ahadi hiyo wiki iliyopita, wakati alipokuwa katika ziara yake wilayani Kishapu na Kahama ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja huku akifanya mikutano ya hadhara na kutembelea walengwa wa TASAF.

Alisema nyumba aliyonayo mlengwa huyo sio imara na kuahidi kutoa Shilingi milioni tatu ili ajengewe nyumba ndogo ya kisasa ambayo itamsaidia kumstiri na wajukuu wake wawili.

Katika hatua nyingine Mjema, akiwa wilayani Kahama aliahidi kutoa fedha Sh. 500,000 kwa ajili ya kumsaidia hali ya maisha Bibi Zainab Masolwa mkazi wa Bugarama wilayani humo, ambaye ana maisha magumu na kuagiza aingizwe pia kwenye mfuko huo wa kunusuru kaya maskini (TASAF).

Aliwataka walengwa wote wa TASAF mkoani humo, wazitumie fedha hizo za ruzuku kwa malengo yaliyokusudiwa na sio kuzitumia kwa mambo ya hamasa, ili ziwatoe kwenye umaskini ikiwamo kuwekeza kwenye mifugo na kilimo.

Nao walengwa hao wa TASAF walioahidiwa kupewa msaada, akiwamo Mwashi Masanja, alisema nyumba hiyo itamsaidia kuishi salama na wajukuu wake wawili.

Alisema nyumba hiyo ya tope ambayo anaishi sasa aliijenga kupitia fedha hizo za TASAF na kuezeka bati na kumshukuru Mkuu wa Mkoa kuahidi kumjengea nyumba nyingine ya kisasa.

Kwa upande wake, Mratibu wa TASAF Mkoa wa Shinyanga, Dotto Maligisa, alisema katika utekelezaji wa mpango huo wa kunusuru kaya maskini TASAF 111 awamu ya pili mkoani humo, kwa kipindi cha kuanzia (2020-2023), kuwa jumla ya kaya 14,785 zimekidhi vigezo na kuingizwa kwenye mpango huo na kaya 7,155 zilikosa sifa na kuondolewa.

Pia aliwataka waratibu wa TASAF ngazi ya halmashauri, kuwa kabla ya kuwapatia fedha za ruzuku walengwa hao, wawe wanawapatia elimu ya matumizi sahihi, ikiwamo kuwekeza kwenye miradi yenye tija ambayo itawatoa kwenye umaskini.

Alitaja mafaniko aliyoyapata kupitia utekelezaji wa mpango huo, kuwa tangu mwaka 2015 hadi 2021, kaya 24,600 zimejiunga na Bima ya Afya (CHF) iliyoboreshwa, 22,411 zimeanzisha miradi ya kiuchumi, 4,119 zimeboresha makazi yao na kujenga nyumba za bati na zingine kula milo mitatu kwa siku.

# DCDO kutekeleza mradi hedhi salama

**Na Salome Mwasamale**

TAASISI ya watu wenye ulemavu wa macho ya Disabilities Community Development Organization (DCDO), inatarajia kutekeleza mradi wa hedhi salama kwa watoto wa kike wenye ulemavu utakaoenda na utoaji wa karatasi ngumu za kusomea na fimbo nyeupe kwa jamii hiyo wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 15.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Hamisi Uchuro, alisema mradi huo unatarajia kuanza katika shule nne za watu wenye ulemavu zilizoko jijini Dar es Salaam na baadaye utaendelezwa katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Alizitaja sababu za kuanzishwa kwa mradi huo kuwa ni kutokana na changamoto mbalimbali wanazokutana nazo watoto wa kike wenye ulemavu wakati wa hedhi hali inayosababisha kushindwa kujiamini na kutofikia ndoto zao.

Aliitaja sababu nyingine kuwa ni hali mbaya ya kiuchumi wanayoipitia watu wenye ulemavu na kusababisha kushindwa kumudu kununua mahitaji muhimu ikiwamo fimbo, karatasi za kusomea mat-ibabu na chakula.

"Familia nyingi za watu wenye ulemavu zinaishi katika mazingira magumu na kujikuta wakishindwa kumudu gharama za maisha ikiwamo za ununuzi wa karatasi na fimbo kwa ujumla ndiyo maana taasisi yetu imeona ni vyema iwasaidie japo hivyo vitu muhimu vitakavyo wasaidia katika masomo yao," alisema.

Katibu wa taasisi hiyo, Idd Mshindo alisema mradi huo ni endelevu kwa kuwa shule za watu wenye ulemavu zimesambaa nchi nzima na wote wanahitaji msaada wao.

Aidha, alizitaja sababu za mradi huo kuanzia jijini Dar es Salaam kuwa ni fursa ya kipekee kwa shule zilizoko hapa kwa kuwa ndipo ilipo makao makuu ya DCDO na waliona ni vyema kutoa nafasi ya upendeleo kabla ya kwenda mikoani.

Akizungumzia kuhusu fimbo nyeupe alisema ni mradi muhimu kwa wasioona kwa kuwa hiyo ndiyo miguu yao na aliwaomba Watanzania kuitambua na kuiheshimu fimbo hiyo ambayo ndiyo msaada wa maisha yao.

"Tunawaomba Watanzania kwa ujumla waitambue fimbo nyeupe wanayotumia walemavu kutembelea kwa kuwa hiyo ndiyo miguu yetu wanapoiona iwe barabarani au njiani waiheshimu na kuithamini ikiwezekana watoe msaada," alisema.

Naye mtunza hazina wa taasisi hiyo, Kessy Shaban, aliyaomba mashirika na wadau mbalimbali kujitokeza kusaidia taasisi hiyo ili kufanikisha mradi huo na kufikia malengo ya kuwafikia wenye ulemavu kote nchini ili na wao wasome kwa furaha na amani na kufikia ndoto zao.




Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, akikabidhiwa viti na meza 100 vyenye thamani ya Sh. milioni 10 na Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, kwa ajili ya Chuo cha Afya Mpanda, viti hivyo ni msaada kutoka Benki ya NMB Kanda ya Magharibi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajiunganishia umeme kinyemela kwenye 'transformer'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kijiji na Kata ya Mbika, Halmashauri ya Ushetu wilayani hapa, wameanzisha utaratibu wa kujiunganishia kinyemela umeme kutoka kwenye 'transformer' iliyoko kijijini hapo kutokana na kukatika mara kwa mara na kukwamisha shughuli zao.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Faida Lutenge, alisema hayo wakati akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kuwa kumeibuka mafundi vishoka wanaowasha umeme kutoka kwenye transformer pindi umeme unapokatika hali ambayo inahatarisha usalama wao.

Alisema transformer iliyoko kijijini hapo ni ndogo na inazidiwa na matumizi ya wananchi wa kijiji hicho kutokana na umeme mwingi kutumika kwenye viwanda na kusababisha umeme kuwa mdogo kwenye makazi yao na wakati mwingine kukatika mara kwa mara.

"Kijiji chetu kina viwanda vya kuchakata nafaka, transformer iliyoko ni ndogo na haiwezi kuhimili matumizi ya umeme katika viwanda vilivyoko, ili kuondoa changamoto hii inatakiwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuja kubadilisha transformer hii na kuweka kubwa zaidi," alisema Lutege.

Vile vile, alisema tatizo hilo lina muda mrefu na lilianza kwa mara ya kwanza tangu kijiji hicho kilipounganishiwa huduma hiyo na kwamba kila siku amekuwa akitoa taarifa TANESCO, ili kwenda kuibadilisha lakini hadi sasa hawajatekeleza na wananchi wanaendelea na utaratibu wao.

Alisema viwanda vingi vinafanyakazi ya kuchakata nafaka nyakati za usiku ili kuepuka kukatika kwa umeme, lakini hautoshi na kukatika jambo linaloleta kero kwa wananchi.

Naye William John mkazi wa eneo hilo, alisema umeme unakatika mara kwa mara na kukwamisha shughuli zao na kuwasababisha kwenda kuwasha umeme kwenye switch ya transformer licha ya kuwa ni hatari kwao na kuwaomba TANESCO kufika na kuibadilisha inayoweza kuhimili matumizi yaliyoko.

Kwa upande wa Meneja wa TANESCO Kahama, Mhandisi King Fokanya, alisema transformer iliyoko kijijini hapo ina ukubwa wa KVA 50 hali ambayo haiwezi kukidhi mahitaji ya wananchi na hivi karibuni watakwenda kufunga mpya yenye ukubwa wa KVA 200 ambayo itakidhi mahitaji ya wananchi.

Kuhusu umeme kuwa mdogo, alifafanua inatokana na matumizi makubwa yaliyoko kuliko ukubwa wa transformer iliyoko.

Aidha, Fokanya aliwataka wananchi kuacha tabia ya kujiunganishia umeme kinyemela, kwa kuwa kufanya hivyo ni wizi na kwamba watakaobainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

# Wachimbaji wadogo watajwa chanzo ukatili kijinsia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MATUKIO ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto wilayani Kahama mkoani Shinyanga, yanaendelea kushika kasi baada ya wachimbaji wadogo kuwashambulia wake zao kwa vipigo hasa wanapopata fedha baada ya kuuza madini ya dhahabu.

Mkaguzi wa Jeshi la Polisi na Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wilayani hapa, Tiho Mastu, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake kuwa vitendo vya kikatili vimezidi katika maeneo ya wachimbaji wadogo ikilinganishwa na maeneo mengine.

Alisema, tangu kuanza kwa mwaka huu, jumla ya matukio 14 ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto yameripotiwa na kwa asilimia kubwa yanafanywa na wachimbaji wadogo baada ya kuuza madini ya dhahabu na kupata fedha na ulevi uliokithiri.

Masatu alisema, ili kuondoa matukio ya namna hiyo elimu ya ukatili wa kijinsia inahitajika kuwasaidia kinamama na watoto wanaopata shida katika matukio hayo na kuyaomba mashirika yasiyoyokuwa ya kiserikali kuongeza nguvu katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

"Vitendo vya wanaume kuwapiga wake zao vimeshamiri katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu, mfano katika machimbo madogo ya madini Mwime, wanawake wanafanyiwa vitendo vya kikatili na wanaume zao na kila siku wanakuja kuripoti ofisini kwangu," alisema Masatu.

"Mwaka 2019 kulikuwa na tukio moja la mzazi kumwingilia mwanawe kimwili mwenye umri wa miaka 15 nyakati za usiku bila ya yeye kujitambua katika ndoto na kesi hiyo bado tunaishughulikia na wananchi kutambua imani potofu isiwe sehemu ya maisha yao," aliongeza Masatu.

Pia alisema, katika kipindi cha mwaka huu matukio matatu ya ubakaji na moja la kutorosha mwanafunzi yamesharipotiwa, tabia hizo zimekuwa zikiendelea kuongezeka kutokana na maadili ya vijana kuiga yasiyokuwa na faida yoyote yanayoleta madhara makubwa katika familia.

Hata hivyo, Masatu alisema, mipango iliyopo kwa sasa ndani ya dawati la jinsia ni kuwapatia elimu ya ukatili wa kijinsia na madhara yake wachimbaji wadogo katika maeneo yote ya migodi midogo, wengi wa wanawake wanaofanyiwa vitendo hivyo wanaishi mazingira magumu hata nyumba zimejengwa kwa maturubai. Naye Godfrey Shukuru, mchimbaji mdogo wa Mwime alisema, wanaofanya vitendo vya kikatili migodini ni wale walioacha wake zao mikoani na kukimbilia migodini kutafuta maisha, wanapopata mali huacha wake zao waliwapata migodini na kurejea kwa wake zao mikoani.

Alisema, kama mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotetea haki za wanawake na watoto kwa kushirikiana na dawati la jinsia watatoa elimu ya ukatili na madhara yake, wachimbaji ambao walikuwa na dhana ya kukimbia familia wataacha na kuachana na vitendo hivyo kwa sababu vinatokea baada ya familia kuongezeka.

# Mkulima mbaroni tuhuma rushwa ya Sh. 300,000

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora imemfikisha Mahakama ya Hakimu Mfawidhi wilayani humo, mkulima wa Kijiji cha Isenegeja, Kata ya Mwisi, Richard Masanja (44) kwa tuhuma za kutoa rushwa ya Sh. 300,000 kwa Katibu wa Baraza la Ardhi la Kata ya Mwisi, Philipo Isaya Mabula.

Ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Mazengo Joseph, kuwa Januari 12, mwaka huu, majira ya asubuhi katika ofisi za Baraza la Ardhi Kata ya Mwisi, mshtakiwa huyo alikamatwa na maofisa wa TAKUKURU akitoa rushwa hiyo.

Mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Igunga, Juhudi Stephen Mdonya, mwendesha mashtaka alidai, mshtakiwa huyo alitoa kiasi hicho cha fedha kama kishawishi ili Katibu wa Baraza hilo aweze kumpa upendeleo katika kesi yake inayomkabili ya mgogoro wa ardhi dhidi ya Mhoja Ntima, kwenye baraza hilo.

Aidha, Mzengo alidai pia mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2019 inayozuia kutenda makosa kama hayo.

Baada ya kusomewa shtaka, hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.

Mshtakiwa huyo alipelekwa mahabusu baada ya wadhamini kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ya Shilingi milioni mbili za maandishi pamoja na hati ya nyumba.

Kesi hiyo itatajwa Januari 28, mwaka huu.




Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jamal Katundu (kulia), akimkabidhi namba ya bajaji mtumishi mwenye ulemavu Joilia Msuya ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi na Marekebisho Masiwani Tanga, yenye thamani ya Sh. milioni 8.1 iliyotolewa na Kampuni ya ASA Microfinance jana. Kushoto anayeshuhudia ni Meneja wa ASA Tanga, Mohamed Zakir Hussein. **PICHA: OSCAR KASIMIRI**

# Wananchi Mbwawa waanza kupata majisafi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

HATIMAYE wakazi wa kata ya Mbwawa, Halmashauri ya Kibaha, wameanza kunufaika na majisafi ya kisima baada ya jitihada za Diwani Judith Mluge.

Akizungumza na Nipashe juzi mjini hapa, Diwani Judith, alisema kwa zaidi ya miaka 10 wananchi wa Mbwawa shule na Mkoleni, wanatumia maji ya visima ambayo hayakuwa salama kwa afya zao.

Alisema kutokana na adha hiyo baada ya kupata nafasi ya kuwa diwani wa kata hiyo, alitafuta wafadhili wa kuchimba visima wakati miradi ya maji ya DAWASA ikiendelea.

Alisema wafadhili hao walipatikana kwa msaada wa Naibu Meneja wa Shule za Feza, Ali Akkiz na kufanikisha uchimbaji wa visima 11 kwenye mitaa yote minne ya kata hiyo, mradi ambao umetekelezwa na wafadhili tofauti.

Upatikanaji wa visima hivyo umeondoa usumbufu waliokuwa wakikumbana nao wanawake wa kata hiyo, pia wanafunzi ambao walikuwa wakilazimika kwenda shule na vidumu vya miji.

Aliwashukuru wafadhili hao huku akiwaomba wananchi kuendeleza ushirikiano katika kutatua ukosefu wa huduma za kijamii kwenye kata hiyo.

"Uchimbaji wa visima ulianza mwanzoni mwa Januari na mpaka sasa yapo maeneo tayari yananufaika na maji zikiwamo shule ambazo hapo awali hazikuwa na huduma hiyo na kusababisha wanafunzi wanapoenda shule kwenda na maji kila siku," alisema.

Kwa mujibu wa Judith, kwa sasa wanatafuta fedha kwa ajili ya kuunganisha maji hayo kwenye vyoo ili wanafunzi wayapate kwa urahisi.

Judith ni diwani pekee mwanamke kati ya 14 wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, ambaye katika kata ya Mbwawa tayari amefanikisha ujenzi wa ofisi ya kata, upatikanaji wa eneo la ujenzi wa kituo cha afya.

Aidha, amefanikisha upatikanaji wa eneo la kituo cha polisi, wafadhili walichimba visima kukabiliana na kero ya maji na sasa pia anapambana kupata kivuko kwa wananchi wanaojishughulisha na kilimo karibu na Mto Ruvu.

# BRELA yapigia debe urasimishaji biashara

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imewataka wafanyabiashara kujitokeza kwa wingi kurasimisha biashara zao kwa kuwa kuna faida.

Rai hiyo ilitolewa jana na Ofisa Usajili kutoka BRELA, Yusuph Mwakasyafuka, wakati wakiwapa mafunzo wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM) kuhusu namna ya kuingia katika ujasiriamali kabla au baada ya kumaliza masomo yao.

Mwakasyafuka alisema urasimishaji wa biashara ni hatua ya kwanza na muhimu katika uanzishaji na uendelezaji wa biashara hatua ambayo ikirukwa inaweza kusababisha kuyumba au kuanguka kwa biashara baadaye.

"Watu wengi wanafanya makosa wakati wa uanzishwaji wa biashara, mathalani kuanzisha na kutangaza biashara ambayo haijasajiliwa ni kinyume na taratibu kwa sababu kwa kufanya hivyo unaweza kuwa unavunja sheria kwa kutumia jina la mtu mwingine bila kujua au mtu mwingine anaweza kulisajili jina hilo na kulifanya lake kisheria," alisema Mwakasyafuka.

Aidha, aliwatoa hofu kuhusu gharama za usajili wa kampuni na kueleza kuwa mtu anaweza kusajili kampuni akiwa na mtaji wa kuanzia Sh. 20,000 na kuendelea na ada za usajili zimegawanyika katika makundi mbalimbali kulingana na mtaji husika.

"Ada za usajili wa kampuni sio kubwa kama watu wengi wanavyodhani na hii ni kwa sababu zimegawanywa kulingana na kiasi cha mtaji mfano kama mtu ana mtaji wa kuanzia shilingi za kitanzania 20,000 hadi 1,000,000 atapaswa kulipa ada ya usajili ya 167,200," alieleza Mwakasafyuka.

Kwa upande mwingine pia kuna fursa ya kurasimisha biashara kwa wajasiriamali ambao hawajafikia hatua ya kufungua kampuni, hivyo wao wanaweza kusajili jina la biashara kama hatua ya kuanzia, ada ya usajili ni Sh. 20,000 pekee.

Kwa upande wa alama za biashara na huduma ambazo hufahamika zaidi kama (logo), mtu anaweza kukamilisha usajili wake kwa Sh. 125,000.

Alisema usajili wa alama hizo una faida lukuki katika soko la ushindani wa kibiashara kwa sababu unasaidia kuitangaza bidhaa husika na kuifanya ifahamike kwa wateja kama ni bidhaa na kama ni huduma kusaidia wale wanaohitaji waweze kuifikia kwa urahisi pale inapohitajika. Naye Mariam Swalehe Said, ambaye ni Mkuu wa Idara ya Uhasibu katika chuo hicho aliipongeza BRELA kwa juhudi zake za kutoa elimu kwa umma na uhamasishaji wa urasimishaji wa biashara kwa sababu ni muhimu kwa vijana ambao wameanza masomo na wanaoelekea kumaliza.

"Elimu hii itawafungulia njia mpya wanafunzi wa chuo, badala ya kusoma masomo darasani pekee sasa wanapata fursa ya kufahamu pia upande wa pili, kuna vitu gani wanapaswa kufanya, nawashukuru sana BRELA kwa elimu hii," alisema Mariam.

Katika urasimishaji wa biashara, BRELA imepewa majukumu kwa mujibu wa sheria kusajili kampuni, majina ya biashara, alama za biashara na huduma, utoaji wa leseni za biashara kundi A, leseni na viwanda.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 18, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI





Ukurasa 12

CHAKUA kinapoamua kukabili kero ya usafiri wa wanafunzi nchini



Ukurasa 14

**Daktari 'roboti' anavyoaminika**

ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Kumbukeni bila misitu maisha yako hatarini

NAMSHUKURU Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa masuala yote anayotujalia kila siku katika kipindi hiki cha mwaka mpya wa 2022. Kwa nyakati tofauti nimekuwa nikieleza umuhimu wa misitu kwa maisha ya Watanzania. Na leo tena naendelea kusisitiza misitu ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya taifa na kwa uhai wa watu na viumbe wa taifa hili.

Misitu ni rasilimali muhimu mno kiuchumi, kimazingira na kijamii. Ina faidi nyingi pengine ambazo zikitajwa au zikiorodheshwa zinaweza kujaza mamia ya vitabu, lakini kikubwa ni kufahamu kuwa inahitajika na ni ya lazima kwa maisha ya kila mmoja, kuanzia binadamu, wadudu na mimea. Lakini ni rasilimali mtambuka kwa sekta nyingine zote muhimu kwa ajili ya ustawi wa kila Mtanzania.

Misitu inamgusa kila mtu, kwanza ni baba wa sekta karibu zote kuanzia afya na tiba, kilimo na chakula, mvua na maji, umeme, upepo, kuchavusha mazao, asali, wanyama pori, mifugo na mbolea ardhini.

Ni chanzo cha hewa safi angani na ardhini, huzuia dhoruba baharini, hasa mikoko ndiyo inayodhibiti mawimbi ya tsunami na vimbunga yasifike mbali na kusababisha madhara kwa binadamu na uwekezaji ukanda wa pwani au ufukweni. Ndiyo inayopunguza joto duniani na kitaalamu huitwa mapafu ya dunia hasa ya Amazoni iliyoko Amerika Kusini na Misitu ya Congo kwa Afrika.



Mikoko inapunguza kasi ya tsunami na vimbunga baharini, kuikata ni kuhatarisha maisha wakati huu wa mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: MTANDAO**

Faida za misitu ni nyingi mno, lakini kwa kujikumbusha mwaka 1961 Tanganyika ilipopata Uhuru eneo la misitu lilikuwa hekta milioni 33.5 na asilimia 50 yake ikiwa ni misitu iliyohifadhiwa kisheria. Ilikuwa ya kijani na iliyokuwa imestawi.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotokana na mradi wa kupima na kutathmini misitu nchini (NAFORMA) zilizotolewa na serikali mwaka 2015, eneo lenye misitu ni hekta milioni 48.1 ikiwa ni ongezeko la takribani hekta milioni 14.6. Kwa takwimu hizo ni rahisi kusema Tanzania ina misitu mingi kumbe sivyo.

Ongezeko linatokana na tafsiri ya neno 'msitu' iliyowasilishwa Umoja wa Mataifa (UN) kuwezesha Tanzania kunufaika na biashara ya gesi ukaa au 'carbon trading'. Hivyo, msitu ulitafsiriwa kuwa "ni eneo lenye miti yenye urefu kuanzia mita mbili na matawi yake au kitaalamu 'crown cover' kufunika asilimia 10 ya hekta moja.

Kabla ya hapo msitu ulijulikana ni eneo lenye miti mirefu zaidi ya mita tano. Kwa tafsiri ya sasa maeneo mengi yaliyofunikwa na vichaka yakatambulika kuwa ni sehemu zenye misitu. Wengi wanaiangalia misitu na miti iliyopandwa kwa kuzingatia magogo, mbao, kuni, mkaa, nguzo na malighafi kwa viwanda vya karatasi wakati misitu ni zaidi ya mahitaji hayo.

**UMUHIMU KWA WOTE**

Ukweli ni kwamba misitu inabeba, kwa kiasi kikubwa, maisha ya Watanzania mijini na vijijini, kinapoongelewa kilimo kijani misitu inachangia sana uwepo wake, mathalani, inarutubisha ardhi au udongo kutokana na majani, matawi, na miti inayozeeka kuanguka na kuoza hivyo kutengeneza mboji.

Kadhalika, misitu huhifadhi nyuki ambao hutengeneza asali na katika kutimiza hili, nyuki hutembelea maua ya miti au mimea mingi hivyo husambaza poleni au chavua kutoka mmea mmoja kwenda mwingine, kwa kufanya hivyo, husaidia mavuno ya chakula na biashara kuongezeka kupitia urutubishaji wa maua.

Huduma hii ya kiikolojia ni muhimu kwa sekta ya kilimo na uzoefu unaonyesha kuwa penye misitu ya asili kunakuwapo, juu na chini ya ardhi, wadudu na viumbe mbalimbali ambao husaidia kufanya twangamotaka (biomass) kuoza haraka na kuchanganyika na udongo kuwa mbolea.

Vilevile, misitu inahifadhi udongo kwa kupunguza kasi ya maji ya mvua na upepo mkali hivyo kuzuia mmomonyoko wa udongo. Wakulima wengi wanafahamu thamani ya udongo wenye mboji ndiyo maana hufyeka misitu kwa ajili ya kilimo. Changamoto ni kuhamahama ili waweze kupata mazao mengi bila kutumia mbolea ya viwandani hivyo

INAENDELEA UK.13

ELIMU NA SABATO KASIKA

# CHAKUA kinapoamua kukabili kero ya usafiri wa wanafunzi nchini

• Kimeunda idara maalum, kugusa shule binafsi

WANAFUNZI wanasoma shule za mijini, wanakumbana na kero mbalimbali, mojawapo ni kukwama usafiri kwa wakati wote wanapokwenda shuleni au kurudi nyumbani, hali inayosababisha washindwe kuwahi vipindi darasani na kuchelewa kurudi nyumbani.

Kero hiyo inachangiwa na baadhi ya madereva na makondakta wa daladala, kuwaacha kwenye vituo kutokana na kulipa nauli ndogo ya Sh. 200 wakati watu wazima hulipia zaidi.

Kutokana na kuendelea kuwapo kwa kero hiyo, Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), kimeanzisha idara ya huduma kwa wanafunzi na watoto ambayo itasimamia haki zao wakiwa vituoni na kwenye magari ya shule binafsi kusaidia kupunguza na hatimaye kuondoa kero kwa wanafunzi mijini.

Adinani Mbezi, ni mkuu wa idara hiyo, ambaye katika mazungumzo yake na gazeti hili, anasema itaanza mchakato wa kukutana na wadau wa usafirishaji wa abiria wiki hii, kwa ajili ya semina, ili kuwekana sawa.

"CHAKUA inatetea abiria wote, lakini imeamua kuanzisha idara maalumu kwa ajili ya wanafunzi na watoto, ambayo itakuwa na jukumu la kuhakikisha hawanyanyasiki wanapotafuta usafiri kwenda shule," anasema Mbezi.

### KUHAMASISHA MABADILIKO

Mbezi anasema, kazi ya idara hiyo ni kutoa elimu kwa makondakta na madereva wa daladala nchi nzima ili watambue umuhimu wa wanafunzi kupata usafiri kwa ajili ya kuwahi shuleni na kufahamu kuwa elimu ndiyo msingi wa maisha.

"Tatizo kubwa linalosababisha kero kwa wanafunzi, ni baadhi yao kutoelewa umuhimu wa wanafunzi kuwahi shule, hivyo na nasi tumeona tuwe na idara ambayo itawaelimisha ili watambue umuhimu huo," anasema.

Anasema, idara hiyo imeweka wawakilishi wake katika miji yote nchini, ambao watahakikisha wanafunzi na watoto hawanyanyasiki wapotafuta usafiri wa daladala na kwamba hilo litafanyika baada ya kuelimisha wahusika.

"Wiki hii tumepanga kukutana na wamiliki wa daladala, vyama vya madereva na makondakta wa Dar es Salaam, katika semina ili kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kuwachukua wanafunzi ili wawahi shule au nyumbani," anasema.



Baadhi ya wanafunzi wakitafuta usafiri. **PICHA: MTANDAO**

> **"Lakini hao CHAKUA wasaidie kuelimisha wanafunzi kujua haki zao wanapokuwa safarini, ili kuepusha manyanyaso wanayopata kutoka kwa baadhi ya makondakta na madereva.**

Mkuu huyo wa idara anasema, baada ya semina hiyo, kitakachofuata ni wafanyakazi wa idara hiyo kwenda kwenye vituo vya daladala kuona kama madereva na makondakta wanazingatia elimu watakayokuwa wamepewa.

"Tunataka kuanzia Dar es Salaam hasa kwenye vituo vyenye matatizo sugu kama Gongo la Mboto, Mbezi Mwisho kwenda Makabe au Mpigi Magoe, wanafunzi wananyanyasika sana, kisha tutakwenda mikoani," anasema.

Mbezi anafafanua kuwa, watafanyakazi wa idara hiyo watashirikiana na askari wa usalama barabarani ili kuwasaidia wanafunzi kuondokana na kero hiyo ambayo bado haijapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

### SHULE BINAFSI ZIMO

Mbezi anaongeza kuwa jukumu jingine la idara hiyo ni kuzifikia shule binafsi na za serikali zinazotoa usafiri wa wanafunzi, kuhakikisha kero zinazopata wanafunzi wanaotumia usafiri huo zinakwisha.

"Kwenye shule hizo nako kuna kero zake zikiwamo za wanafunzi kujazana kwenye mabasi na wengine kubebana, hali ambayo si salama kwao, hivyo tumeona nasi tushiriki kwa ajili ya usalama wa watoto hao," anasema.



Mkuu wa Idara ya Huduma ya Usafiri kwa Wanafunzi kutoka CHAKUA Adinan Mbezi.

Anasema changamoto ya kuwapo na magari yanayoharibika kila mara nayo itazungumziwa ili wanafunzi wawe salama ndani ya vyombo vya usafiri

Mkuu huyo wa idara anasema, CHAKUA inatarajia kusambaza waraka wa serikali katika shule hizo, ambao unahusu kumsafirisha mwanafunzi akiwa salama aendapo shuleni na akirudi nyumbani.

"Tukiwa wadau wa usafiri tumeona tushirikiane na serikali katika mambo hayo kwa ajili ya usalama wa watoto wetu, na kama wahusika watakaokaidi, itabidi vyombo vya dola viwashurutishe," anasema.

Anasema, mtindo wa kujaza wanafunzi katika basi una madhara mengi yakiwamo ya kupata ajali au kusababisha kuambukizana ugonjwa UVIKO- 19, na kwamba wao kama wadau hawataki hilo litokee.

### ELIMU YA CORONA

Mwenyekiti wa CHAKUA Taifa, Hassan Mchangama, anasema, chama hicho mbali na kutetea abiria, kimejikita pia kutoa elimu ya UVIKO-19 kwa wasafiri wote wakiwamo wanafunzi.

"Tumeanzia mkoani Dar es Salaam ambapo tunakuwa kwenye vituo mbalimbali vya daladala tukihamasisha watu kuzingatia mwongozo wa Wizara ya Afya na pia kupata chanjo," anasema Mchanjama.

Anasema, mwongozo unawataka abiria kutojazana kwenye daladala, bali wakae kulingana na idadi ya viti, kuvaa barakoa, kunawa majitiririka, pia kila kituo kuwa na tangi la majitiririka na vitakasa mikono.

### UMBALI CHANGAMOTO

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Jitihada ya Dar es Salaam, Augustine Byalile, anasema ipo haja kwa wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao katika shule za jirani ili kupunguza usumbufu wa usafiri.

Anasema, hatua hiyo itasaidia kupunguza kero wanazokumbana nazo wanapotafuta usafiri wa kwenda shule hali inayosababisha wachelewe baadhi ya vipindi vya masomo hasa asubuhi.

"Shuleni Jitihada kulikuwa na tatizo hilo, lakini kwa sasa limeisha, kutokana na kwamba wanafunzi wanaosoma hapa, wanatoka maeneo ya jirani, hivyo uchelewaji unaosababishwa na makondakta umekwisha," anasema Byalile.

Aidha, akizungumzia hatua zinazochukuliwa na CHAKUA, anasema zinaweza kuleta mabadiliko kwenye usafiri, hasa kwa wanafunzi iwapo wadau watapokea elimu watakayopewa na kuifanyia kazi.

"Lakini hao CHAKUA wasaidie kuelimisha wanafunzi kujua haki zao wanapokuwa safarini, ili kuepusha manyanyaso wanayopata kutoka kwa baadhi ya makondakta na madereva," anasema.

Anasema wakijua haki zao kwa mujibu wa sheria watachukua hatua na mambo hayo yanaweza kukomeshwa.

# Bila misitu maisha yako hatarini

INATOKA UK.11

kusababisha misitu itoweke kwa kasi.

Halikadhalika misitu husaidia udongo uwe na unyevunyevu kwa muda mrefu zaidi ukilinganisha na maeneo yaliyo wazi, aidha ndani ya misitu ipo miti na mimea ambayo mizizi yake hufyonza 'naitrojeni' kutoka hewani na kusaidia kurutubisha udongo. Miti aina hiyo ni viwanda vya kutengeneza mbolea ardhini na kuongeza tija hivyo kilimo - misitu kizingatiwe. Rasilimali misitu pia ni muhimu kwa mifugo maana kwenye misitu hupatikana chakula na maji na umuhimu wa misitu kwa mifugo unaongezeka zaidi nyakati za ukame.

**ZILIKO DAWA**

Kadhalika, misitu inachangia katika usalama wa chakula kwa kuzingatia upatikanaji wa matunda na mboga asilia pamoja na wadudu mbalimbali wanaoliwa, ndiko unakopatikana uyoga hasa majira ya mvua kadhalika misitu ni makazi ya wanyamapori ambao ni muhimu kwa utalii pia wananchi hupata kitoweo wengine kuuza kupata fedha.

Kwa upande mwingine, misitu inatumika kupata dawa za asili ambazo hutibu magonjwa mbalimbali ya binadamu na mifugo. Isitoshe, viwanda vingi duniani, msingi wake muhimu ni misitu ambako hupata vinasaba vya dawa na vipodozi mbalimbali. Inapotokea ugonjwa usioeleweka kisayansi kama COVID-19, kimbilio ni matumizi ya mitishamba. Kwa hali hiyo sekta ya afya na tiba inafungamana sana na misitu.

**VYANZO VYA MAJI**

Kwa upande wa maji misitu inachangia kwa kiasi kikubwa. Maeneo yasiyo na misitu huwa makame sana na kusababisha upatikanaji wa maji kuwa shida. Kwanza, misitu kwenye maeneo yenye miinuko husababisha upepo wenye unyevu kutoka baharini, kupungua kasi yake na hatimaye kutengeneza mawingu mazito kusababisha mvua kunyesha.

Kadhalika, maji ya mvua huweza kuingia ardhini na hatimaye kuwa chanzo kikuu cha mito, kwa mfano, misitu katika milima ya Uluguru ni chanzo muhimu cha Mto Ruvu. Karibu mito mikubwa nchini vyanzo vyake ni katika misitu iliyo katika Milima ya Tao la Mashariki.

Misitu ni uhai kwa maana hewa safi ya 'oksijeni' kila mtu anayayovuta kila siku inatokana na misitu au miti. Binadamu anapopumua hutoa gesiukaa (CO2) na miti huitumia na kutoa 'oksijeni' (O2) ambayo ni msingi wa uhai wa kila mtu.



Misitu ni makazi ya wanyama, vyanzo vya maji na dawa. Miti na mimea ni malighafi zinazozalisha dawa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Pamoja na umuhimu huo, bado kasi ya kutoweka misitu na uoto wa asili ni kubwa kati ya hekta 372,000 hadi 500,000 kwa mwaka.**



**BILA MISITU NI KIFO**

Kukosekana matumizi endelevu ya misitu kunahatarisha uhai wa wanadamu, wanyamapori, mimea na viumbe wengi karibu wote. Mfano misitu na wanyamapori walioko Serengereti na Selous inapoathirika wanyamapori pia hudorora kwa kukosa chakula na maji hivyo kusababisha utalii nchini kuyumba.

Kwa upande mwingine, misitu hutumika kwa mafunzo hususan, kujifunza ikolojia ya misitu na umuhimu wake kwa maisha ya kila siku. Vilevile, vyuo hutumia misitu kufundisha wataalamu kivitendo pamoja na mbinu za uhifadhi na kufanya tafiti mbalimbali kwa manufaa yetu.

Isitoshe, misitu ni sehemu muhimu sana katika mazingira yanayomzunguka binadamu na bioanuwai. Dunia sasa inalia na changamoto za ongezeko la joto na mabadiliko ya tabianchi kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu zisizoendelevu viwandani na kwenye misitu. Nchi zilizoendelea zinachangia sana kuwapo kwa gesiukaa angani. Kiwanda cha kutumia gesiukaa ni misitu na mimea mingine hivyo kupungua misitu kunachangia uwepo kiwango kikubwa cha gesiukaa angani.

Athari za mabadiliko ya tabianchi ni nyingi ikiwamo ongezeko la ukame, kuzuka kwa wadudu na magonjwa mbalimbali yanayodhuru mimea, mazao, wanyama na binadamu hivyo kutishia uhai wa kila mmoja. Inabidi juhudi kubwa zifanyike kuhifadhi misitu na kupanda miti mingi kwa faida ya vizazi vya sasa na baadaye.

**NYUMBA YA NISHATI**

Misitu ni chanzo muhimu cha nishati nchini kwa sababu inachangia sana kwenye upatikanaji wa maji ya kuzalisha umeme pia ikiwa ni asilimia 80 ya nishati inayotumika nchini kupitia kuni na mkaa. Misitu pia ni rasilimali muhimu vijijini ambako makabila mbalimbali hutumia misitu kwa matambiko na msuala ya kimila na kifamilia ikiwamo sehemu za kuabudia.

Kadhalika, misitu hutumika kama sehemu muhimu za maziko kifamilia au kwa kijiji. Pamoja na umuhimu huo, bado kasi ya kutoweka misitu na uoto wa asili ni kubwa kati ya hekta 372,000 hadi 500,000 kwa mwaka. Hii inatokana na misitu kutopewa umuhimu wa kutosha kama ilivyo kwa sekta za afya, maji, elimu, kilimo, miundombinu.

Iwapo sekta hizo zinagusa maisha ya Watanzania misitu nayo inagusa sana maisha ya kila Mtanzania na uchumi wake. Kimsingi misitu ya asili haijasimamiwa ipasavyo isipokuwa shughuli zinafanyika kisiasa zaidi kuliko kitaaluma. Hali ya misitu ya asili siyo nzuri na madhara yake kwa taifa yataendelea kuwa makubwa kama hatua za kuiunganisha misitu pamoja na 'sekta nyeti' za kitaifa hazitachukuliwa. Wataalamu wajitahidi kutimiza majukumu yao kufuatana na misingi ya kitaaluma na kuhakikisha rasilimali misitu inakuwa ya manufaa kwa Watanzania wote.

***Dokta Felician Kilahama ni Mkurugenzi mstaafu wa Misitu na Nyuki.***

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

# Daktari 'roboti' anavyoaminika

• Operesheni ngumu huifanya kwa weledi, ufanisi mkubwa



Robo dokta akiwa kazini, ni mashine za roboti zinazofanyakazi katika chumba cha upasuaji kufanikisha operesheni mbalimbali. **PICHA: MTANDAO**

ROBOTI ni neno lenye asili ya Kirusi 'robota', likimaanisha 'utumwa au kufanyishwa kazi kwa nguvu tena kwa kulazimishwa. Dhana hiyo ya robota leo imekwenda mbali. Ipo katika sekta zote na imekuwa ni mbadala kwenye kufanyakazi hatari ambazo zingetishia uhai wa mtu.

Robota ilipochukuliwa na kutumiwa kwenye maabara za kuzalisha kiteknolojia ilitengeneza mashine zinazofanyakazi badala ya binadamu na ndizo zinazotumika duniani leo hasa kwenye mataifa yaliyoendelea, zikisifiwa kwa ufanisi mkubwa.

Roboti haichoki, haihitaji mshahara, bima ya afya, mfuko wa hifadhi ya jamii na katika ufanisi inafanyakazi kubwa kuliko binadamu.

Katika sekta ya afya, mashine hizo zimetia fora kwenye matibabu, kwa mfano kuna teknolojia ya kutumia mashine hizo kwenye upasuaji au operesheni mojawapo ni roboti ya 'da Vinci Surgical System' inayowawezesha madaktari kufanya operesheni ngumu, zenye kuhofisha, lakini zinapotumiwa hufanyika kwa umahiri, ufanisi na weledi mkubwa.

Roboti ya tiba ya mfumo wa upasuaji ya 'da Vinci' inatumiwa kikamilifu katika upasuaji wa aina nyingi ikitajwa kuwa ni salama, ina ufanisi kwenye aina mbalimbali za matibabu ya moyo, figo, mishipa ya fahamu na viungo vingine vya ndani, ikifanikisha kazi kwa umakini wa hali ya juu.

> **Nchini Marekani operesheni tatu kati ya nne za saratani ya tezi dume siku hizi zinafanywa kwa kutumia roboti ya matibabu ya da Vinci.**

Duniani leo kuna zaidi ya roboti 1,700 za mfumo wa da Vinci zilizofangwa katika hospitali mbalimbali.

Halikadhalika, wagonjwa zaidi ya 775,000 duniani kote wamewahi kufanyiwa upasuaji kwa njia za roboti hizo wakiwamo wenye matatizo ya moyo, njia ya mkojo, maradhi ya kinamama, wenye magonjwa ya watoto na saratani.

Nchini Marekani operesheni tatu kati ya nne za saratani ya tezi dume siku hizi zinafanywa kwa kutumia roboti ya matibabu ya da Vinci.

### FAIDA KITABIBU

Kwa ujumla roboti katika tasnia ya matibabu, inazidi kupanuka. Hutumiwa kwenye upasuaji, ikiwa na vifaa vya kisasa ambavyo huruhusu shughuli ngumu ya operesheni kufanyika na kufanikiwa kukiwa na makosa ya kiwango kidogo (machache) kuliko ambavyo ingetokea kama upasuaji ungefanyika kwa mikono ya binadamu.

Visu vya mpasuaji roboti huingia katika maeneo ya mwili ambayo haingewezekana kufanya kazi hiyo bila teknolojia hiyo.

Roboti zinaweza kuwa msaada katika kazi ya wataalamu wa afya, kusaidia na kutoa huduma nyingi zaidi ya kile ambacho wataalamu au binadamu wangeweza kufanya hospitalini.

Takwimu kutoka Vituo vya Udhibiti na Kuzuia Magonjwa vya Marekani zinaonyesha kuwa kati ya wagonjwa 25, mmoja atapata maambukizi yanayotokana na kulazwa wodini kama 'staphylococcus aureus' maradhi yanayoshambulia ngozi au njia za juu za hewa, na 'clostridium difficile' vimelea vinavyosababisha magonjwa ya tumbo na kusababisha kuharisha na mtu mmoja kufa kati ya tisa wanaoathirika.

Lakini, kwa kutumia roboti mfano 'xenex', mifumo ya kudhibiti maambukizi inadhibiti maradhi, tena imeonyesha kuwa na ufanisi zaidi. Roboti ya xenex zina uwezo wa kuzuia maambukizi ya moja kwa moja, ambayo hutumia mionzi ya 'ultra-violet' kuharibu seli za vijidudu au vimelea na kuua bakteria hao.

Nchini Ubelgiji roboti pamoja na kutumiwa kwenye matibabu zinatumika kama marafiki zikifanyakazi mapokezi, kupokea wateja, taarifa zao na kuwapa maelekezo ya maeneo mbalimbali ya vyumba vya matibabu na huduma.

Faida ni nyingi lakini kikubwa roboti hazichoki na kila wakati zitaweza kupokea wagonjwa na kutabasamu kwa utaratibu ule ule siku zote, hazikasiriki wala kubadilika na zimewekewa mifumo ya kutambua lugha zaidi ya 20, kufahamu jinsi ya mgonjwa na iwapo ni mtoto.

Kwenye uwanja wa matibabu, roboti zinaweza kuchukua nafasi ya waganga wabobezi au madaktari bingwa wa upasuaji kwa usahihi na ufanisi, zinaona kikamilifu, kama binadamu alivyo binadamu hazitetemeki, hazichoki na ni mbadala wa mwanadamu kwenye upasuaji 'thieta'.

Mfumo wa Upasuaji wa da Vinci unamruhusu daktari wa upasuaji kuona eneo kubwa lililokuzwa kwa kutumia teknolojia ya 3D inayokuza picha na vyombo vya matibabu ambavyo vinaweza kuinamishwa na kuzungushwa kwa pembe kubwa zaidi kuliko mikono ya mwanadamu.

Kwa mfumo wa da Vinci, madaktari wa upasuaji wanaweza kufanya operesheni ngumu kwa kukata chale ndogo au tundu dogo (laparascopic) badala ya kukata eneo kubwa, kukata mishipa ya damu na kuhitajika kulishona na kuunganisha tena huku kazi kubwa ya kuzuia uvujaji wa damu ikipasua kichwa.

Roboti ni utaratibu wa asilimia 100 wa kufanyakazi kwa usahihi ambao hapo awali haukuwezekana.

### MBALI NA UPASUAJI

Roboti za matibabu zina matumizi mengine mfano kusafirisha dawa kwa kiwango kikubwa, kufanya vipimo vya maabara bila hofu ya kuambukizwa magonjwa na kuinua na kuwabeba wagonjwa ambao hawawezi kusimama. Kwa utaratibu wa kawaida wagonjwa wasiotembea au kusimama hubebwa kwenye 'strecha' au viti.

Japan, "robobear", roboti katika sura ya kubeba, husaidia kuhamisha wagonjwa kutoka vitanda vyao kwenda kwenye viti vya magurudumu, uso wa roboti hizo wa kirafiki na nguvu huruhusu wagonjwa kuhisi raha na kuepuka uchovu.

Lakini huondoa uchovu wa wafanyakazi wa huduma ya afya, ambao wakati mwingine hulazimika kuwainua wagonjwa hadi mara 40 kwa siku.

Ndani ya eneo hilo kunapatikana Veebot, roboti anayesimamia kutoboa mishipa na kuchukua sampuli za damu kwa usahihi na kwa ufanisi zaidi, ili kuepuka maumivu na hofu ambayo wagonjwa wengi huhisi wakati wanapitia hali hii. Kwa roboti hii, mchakato wa kuchukua sampuli huchukua chini ya dakika moja na ni sahihi kwa asilimia 83.

Linapokuja suala la utoaji wa dawa, roboti pia ni sahihi zaidi. **MITANDAO**



## Wazazi wanaoenda shambani na kuacha watoto bila chakula kukiona

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAMII imetakiwa kutoa taarifa katika Kituo cha Polisi kipindi wazazi wanapoacha watoto wao na kuhamia mashambani bila mahitaji ya muhimu ikiwamo chakula, ili wachukuliwe hatua kali.

Hayo yalisemwa jana wakati wa mkutano wa Mpango Kazi wa Taifa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), ulioandaliwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Women Wake Up (WOWAP) na kushirikisha kamati ya ulinzi wa wanawake na watoto ngazi za kata na vijiji vya Mpwayungu, Chikola na Nagulo Wilaya ya Chamwino.

Ofisa wa Polisi, Emmanuel Maduma, kutoka Kituo cha Polisi cha Mpwayungu, alisema baadhi ya wazazi wanahamia mashambani na kuwaacha watoto bila uangalizi na mahitaji muhimu kama chakula na kusababisha watoto kujiingiza kwenye vitendo visivyofaa.

"Wazazi wakiwaacha bila fedha nenda katoe taarifa polisi atatafutwa mwenyekiti wa kitongoji, atutafitie huyo mzazi aeleze kwa nini hatimizi wajibu wake, tabia hii imeshamiri sana ina inasababisha watoto wengi kuingia kwenye ngono wakiwa na umri mdogo," alisema.

Alisema ifike wakati kila mzazi atambue umuhimu wake katika malezi ya watoto ili kupunguza vitendo vya ukatili.

Mtendaji wa Kijiji cha Mpwayungu, Selemani Kibakaya alisema, msimu wa kilimo unapoanza wazazi wanakuwa na tabia ya kuhamia mashambani na kuacha watoto bila uangalizi wowote.

Alisema kaya nyingi zinaachwa zikiwa na watoto peke yao na hiyo inakuwa ni moja ya njia inayosababisha watoto wa kike kuingia kwenye vitendo vya ngono.

"Unaweza kukuta wazazi wameahamia mashambani wanawaacha watoto hawana unga wala mboga na kufanya watoto kuanza kuhangaika hangaika," alisema.

Kibakaya alisema wazazi wengine hukaa hata miezi mitatu mashambani jambo ambalo ni hatari kwa kuwa watoto huachwa bila kuwa na ulinzi jambo ambalo ni hatari kwa makuzi yao.

Alisema jukumu la malezi ni la wazazi na wanatakiwa kuhakikisha watoto wanakuwa salama muda wote badala ya kuwaacha kwa visingizio kuwa wanakwenda kufanya kazi.

"Tumeshawaambia wazazi kama wanahamia mashambani wafunge nyumba waondoke na watoto wao kwa usalama zaidi kwani hata mimba nyingi za utotoni hutokea wakati wa msimu ya kilimo," alisema.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Mpwayungu, Festo Mwilawi, alisema wazazi wamekuwa wakiacha watoto na kuhamia mashambani.

# Viongozi wa dini waombwa kusaidia jamii kuepuka mauaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, amewataka viongozi wa dini nchini kuisaidia jamii kuacha vitendo viovu vinavyo sababisha uvunjifu wa amani ikiwamo matukio ya mauaji.

Vile vile, alisema mafundisho ya kiroho ni moja kati ya njia muafaka ya kukomesha matukio maovu ndani ya jamii na kuendeleza amani na utangamano.

Waziri huyo alisema takwimu zinaonyesha katika kipindi cha kati ya Januari mosi hadi 15 mwaka huu, takribani vifo 22 vimeripotiwa katika matukio tofauti ya mauaji katika kijamii.

Masauni, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza katika ibada maalumu ya kitaifa iliyoandaliwa na Kanisa Halisi la Mungu Baba kwa ajili ya kuliombea taifa liendelee kuwa na amani.

Ibada hiyo iliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri na iliwahusisha viongozi wa kitaifa wa dini na wananchi mbalimbali.

"Inasikitisha sana kwamba vifo hivyo 22 vilivyotajwa vimetokea katika ngazi za kifamilia kutokana na baadhi ya sababu dhaifu, ikiwamo wivu wa mapenzi, migogoro ya mali, ugomvi wa ardhi pamoja na imani potofu," alisema.

Kadhalika, alisisitiza matukio hayo ya kikatili yanatafsiri kutokuwapo kwa hofu ya Mungu miongoni mwa jamii, hali inayohitaji msaada wa kiroho kutoka kwa watumishi wa Mungu.

Alilipongeza kanisa hilo kwa kuandaa maombi hayo ambayo alisema kimsingi yanasaidia kuchochea amani na mshikamano na utulivu kwa maendeleo ya nchi.

"Tanzania inaendelea kupiga hatua kubwa kiuchumi kutokana na uwapo wa amani kwa muda mrefu sasa ndani ya nchi, lazima sote tusimame pamoja ili amani iendelee kuwapo," alisisitiza.

Alisema serikali inaelewa na kuthamini mchango mzuri unaofanywa na taasisi za dini katika kuisaidia kusambaza huduma muhimu za kijamii kwa wananchi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kanisa hilo Baba Halisi, alisema litaendelea kusimama mstari wa mbele kuliombea taifa pamoja na viongozi wote wa serikali.

"Tumeamua kuandaa ibada hii maalum ya maombi ya kitaifa, ili kurudisha shukrani kwa Mungu Baba kwa kutupa upendeleo mkubwa sana Tanzania wa kuwa na amani na utulivu.

"Tanzania ni taifa baba linalozalisha na kueneza amani kwa mataifa mengine yote duniani, ndiyo maana sote hatuna budi kumshukuru Mungu Baba kwa hili kwa kumtolea yeye (mwenyezi) sadaka maalumu ya shukurani," alisema.

Alifafanua kuwa jukumu la kanisa halikomei ndani ya 'kuta nne' bali linapaswa kuwa na jukumu la kuunganisha na kuhudumia jumuiya nzima na taifa kwa ujumla kupitia kuhubiri neno la kweli ya Mungu.



Uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma ukiendelea na uzoaji wa taka nje ya soko kuu la Majengo jana, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, kuhakikisha maeneo yote ya mji yanakuwa safi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dodoma kutekeleza agizo la usafi endelevu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JIJI la Dodoma kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa limeanza kutekeleza agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango huku Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, akishauri kuhuwishwa kwa sheria ya usafi ya jiji ili kuwe na usafi endelevu.

Dk. Mpango alitoa wiki mbili kuhakikisha taka zote zinaondolewa na kuweka mikakati ya Jiji la Dodoma lionekane safi katika kata na mitaa yote.

Akizungumza wakati wa kikao baina ya uongozi wa mkoa na watendaji wa kata, mitaa na maofisa afya kutoka maeneo yote ya jijini Dodoma, Mtaka alisema suala la usafi linatakiwa kuwa endelevu.

"Tuone namna ya kuhuisha sheria ya jiji kuhusu masuala ya usafi, hata ikibidi zile faini mtu atakaye kamatwa anayetupa taka basi apewe kamisheni na zingine zitumike kuimarisha usafi," alisema.

Pia aliwataka watendaji wa kila eneo la biashara kuweka vyombo ili kudhibiti uzagaaji na utupaji taka ovyo na kuwa historia.

Mtaka alimtaka mkurugenzi wa jiji hilo kuwa mkali kwa watendaji ambao wanafanya kazi kwa mazoea na vituo vya kazi, watendaji wa kata na mitaa ambao utendaji kazi wao umekuwa sio mzuri huku akisisitiza kutoa kipaumbele kwa wale ambao ni watendaji wabunifu.

Pia alisisitiza pindi soko la wamachinga litakapokamilika hakutakuwa na vibanda mtaani na kuwataka watendaji kutoruhusu ujengwaji wa vibanda vipya vya wamachinga katika mitaa yao.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, aliwataka watendaji, maofisa afya na mazingira kufuata sheria za mazingira kwa kutoa faini kama kuna mtu anastahili adhabu hiyo.

"Kuanzia sasa mimi na timu yangu tutaanza kutembea mtaa kwa mtaa kata kwa kata, nyumba kwa nyumba ili kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa maagizo, nisisitize hii hali iliyojitokeza haitajirudia na sitavumilia," alisema.

Mafuru alimwagiza Ofisa Utumishi kuwaandikia barua watendaji wa mtaa na kata ambao wamekaidi kikao alichoitisha cha kuweka mikakati ya kutekeleza agizo la Makamu wa Rais.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, aliwataka maofisa mazingira, maofisa afya na watendaji wote kuwaonyesha wananchi kufanya usafi kwa vitendo.

"Kuna jumla ya watendaji 239 walioajiriwa serikalini sasa kunasababu gani ya jiji lionekane chafu...hapa kuna mahali hatuwajibiki ipasavyo na tumejisahau lazima tujiulize tumefika hapa mpaka viongozi wa juu wanakuja kutukosoa sisi wachafu kwa sababu gani," alihoji.





# CHUTCU kupambana mabadiliko tabianchi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

CHAMA Kikuu cha wakulima wa tumbaku Mkoa wa Kitumbaku Chunya (CHUTCU), kimeanza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuanzisha miradi mbadala ambayo itawasaidia kujiingizia kipato endapo mabadiliko hayo yataathiri mavuno yao.

Chama hicho kinatarajia kuanzisha viwanda viwili, kimoja kitakuwa cha kusindika unga wa sembe na kingine cha kuchuja mafuta ya alizeti miradi ambayo itasaidia kuwaongezea kipato wanachama.

Kaimu Meneja wa chama hicho, Juma Nshishi, alitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mkuu wa kawaida wa wanachama kuwa mchakato wote wa kuanzisha miradi hiyo umeshakamilika.

Alisema chama kinatarajia kuchukua mkopo wa Sh. milioni 367.6 kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo na kilichokuwa kimebaki ni wanachama kuidhinisha mchakato huo kuendelea ili viongozi waende wakakope.

Alisema mpango wa biashara hiyo (BOQ) umeshaandaliwa na wanakusudia kutumia mapato ya ndani ya chama hicho kurejesha mkopo huo na kwa kuanzia chama kimetenga asilimia 12 ya mapato ya ndani kwa ajili ya urejeshaji.

Alisema kiwango hicho kitakuwa kinaongezeka mwaka hadi mwaka kulingana na mapato ya chama hicho na kwamba aina ya mkopo wanaotarajia kuuchukua, chama kitarejesha ndani ya miaka minne.

"Lengo la uwekezaji huu ni kuongeza kipato na kuongeza thamani ya mazao ya wakulima, tumeshaandaa mpango wa biashara na tunajua wapi tutakuwa tunauza na faida itakayokuwa inapatikana, lakini mradi utatusaidia kupata kipato endapo tutapata shida kwenye tumbaku," alisema Nshishi.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Eliezer Fijabo, alisema waliamua kuanzisha miradi hiyo ili kupanua wigo wa kiuchumi badala ya kutegemea kilimo cha tumbaku pekee walime na mazao mengine ambayo yatakuwa yanasindikwa.

Alisema wanakusudia kuanza kuhamasisha wakulima wa tumbaku kulima mazao hayo ambayo ni mahindi na alizeti ili viwanda wanavyokusudia kujenga vipate malighafi za kutosha na kuzalisha bidhaa ambazo zitatosheleza mahitaji ya soko.

Alisema endapo wakulima watakuwa wanategemea kilimo cha tumbaku pekee, wanaweza wakapata hasara na ikitokea msimu ambao hali ya hewa itaathiri kilimo cha zao hilo.

"Kwa sasa tunahamasisha pia wakulima kulima korosho na mazao mengine ya kimkakati ili wasitegemee tu kilimo cha tumbaku, ni kweli kilimo cha tumbaku kinatusaidia, lakini tunaona ni bora tulime na mazao mengine," alisema Fijabo.

Kwa upande wake Mrajisi Msaidizi wa vyama vya Ushirika Mkoa wa Mbeya, Richard Zengo, aliwataka viongozi wa vyama vya ushirika kuzingatia sheria za uwekezaji ili kuepuka migogoro.

Alisema kwa mujibu wa sheria, chama cha ushirika kinapotaka kufanya uwekezaji mkubwa ni lazima kipate kibali kutoka wizarani na kwa vyama vya msingi vinapata kibali kwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika mkoa.



Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonazi, akisoma kipimo kinachoonyesha urefu na ubora wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa katika kituo cha kutolea huduma Rungwa, ikiwa ni ziara ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya mkongo huo kutoka Manyoni, Singida mpaka Kambikatoto mkoani Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yabuni mbinu kukabiliana rushwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya imebuni mbinu mpya ya kutoa elimu ya kukabiliana na vitendo vya rushwa kwa kutumia michezo na vikundi vya skauti ambavyo vitasaidia kusambaza elimu hiyo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Denis Manumbu, aliyasema hayo jana alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuwa taasisi hiyo imekuwa ikitumia mbinu mbalimbali kutoa elimu kwa wananchi.

Alisema kwa sasa wameanzisha mashindano ya michezo mbalimbali kwa kushirikiana na kikundi cha skauti ambayo yatafanyika jijini hapa na watahakikisha elimu ya kupinga rushwa inawafikia wananchi kwa ufasaha.

Alisema wananchi watapatiwa elimu ya kuvitambua viashiria vya rushwa, namna ya kutoa taarifa na kuepuka kwenye vitendo hivyo vinavyochangia kupotea kwa haki.

"Tunataka kila mwananchi ajue madhara ya rushwa kwenye shughuli ya aina yoyote, tumeamua kutoa elimu kwa wananchi kwa njia hii kwa sababu michezo inapendwa na kundi kubwa la watu na hivyo mashindano haya yatakusanya wengi na tutatoa elimu," alisema Manumbu.

Aliwataka wananchi wa jiji hilo kujitokeza kwa wingi kwenye viwanja vitakavyoainishwa kwa ajili ya kushiriki michezo hiyo na kupata elimu ya rushwa.

Vilevile, aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kushirikiana na taasisi hiyo kwa kuwapa taarifa za vitendo vya rushwa ili vidhibitiwe kabla havijaleta madhara kwenye jamii.

**Alisema wananchi watapatiwa elimu ya kuvitambua viashiria vya rushwa, namna ya kutoa taarifa na kuepuka kwenye vitendo hivyo vinavyochangia kupotea kwa haki.**

# RUWASA yaokoa bil. 1/- mikataba miradi ya maji

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WAKALA wa Maji Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Songwe, umeokoa zaidi ya Shilingi bilioni moja zilizokuwa zinapotea kwenye mikataba ya ujenzi wa miradi 13 ya maji halmashauri zote za mkoa huo, ili kuwasogezea wananchi huduma hiyo muhimu.

Mkoa huo umepatiwa fedha na Serikali Kuu zaidi ya Sh. bilioni 12.25 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo na kabla ya kusaini mikataba na makandarasi watakaotekeleza miradi hiyo, wahandisi wakaamua kupitia upya gharama za kila mradi.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Songwe, Mhandisi Charles Pambe, alisema wakati wanapitia mikataba hiyo waliangalia hali halisi ya utekelezaji wa miradi katika mkoa huo na wakaanza kupunguza fedha hizo mpaka wakabakiwa na Shilingi bilioni moja.

Alisema baadhi ya makandarasi waliweka gharama kubwa kuliko hali halisi ya utekelezaji na ndipo wakaamua kuziboresha gharama hizo.

"Fedha hizo tunakusudia tuzitumie kwenye shughuli zingine za maendeleo, tulizipunguza kwenye mikataba hiyo kwa sababu tunazijua gharama za ujenzi wa miradi kwenye mkoa wetu, tunajua gharama za kuchimba mitaro na kujenga matangi, kwa hiyo hatuwezi kudanganywa," alisema Pambe. Akishuhudia utiaji saini mikataba hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, aliwapongeza wahandisi wa mkoa huo kwa kufanya ukaguzi wa mikataba hiyo na kuokoa fedha hizo ambazo zingepotea kwenye utekelezaji wa miradi hiyo.

Aliwataka wasimamizi wa miradi kuwa makini kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyoendana na gharama halisi za miradi ili kuepuka kutekelezwa chini ya kiwango.

Mgumba alisema mara nyingi ubadhirifu wa miradi huwa unaanzia kwenye ununuzi ya vifaa na kuwataka wataalamu kuwa makini kwenye kipengele hicho ili kulinda fedha za kitanzania zisipotee na miradi itekelezwe kama serikali inavyokusudia.

"Nawapongeza sana kwa utekelezaji wa miradi hii, tungesaini miradi hii na kuanza utekelezaji bila kufanya mapitio fedha hizi zingepotea, sasa nawaomba tuendeleze utaratibu wa kukagua utekelezaji wake," alisema Mgumba.

Mwakilishi wa makandarasi waliopata zabuni za kutekeleza miradi hiyo, Fedrick Luvinga, aliahidi kutekeleza miradi hiyo kwa ufanisi na kwa kuzingatia gharama halisi za miradi.

Alisema mikataba hiyo waliipata kwa kuzingatia vigezo ambavyo vilikuwa vimewekwa na mkoa huo na kwamba watahakikisha wanaitendea haki miradi hiyo kwa kuitekeleza vizuri.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidalya, aliahidi kuwapa ushirikiano makandarasi hao walioshinda zabuni za ujenzi wa miradi hiyo ili kusiwapo na vikwazo vya aina yoyote ambavyo vitasababisha miradi kukwama.

Aliwataka makandarasi hao kuhakikisha wanafanya kazi kwa kuzingatia taaluma zao ili miradi watakayotekeleza ibaki alama kwa wananchi katika kipindi kirefu.





## Wafanyabiashara kufanya malipo kielektroniki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imeanzisha mfumo wa kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki kwa wafanyabiashara hatua ambayo itasaidia kudhibiti mapato.

Hayo yalisemwa jana na Kamishna wa Bodi ya Mapato, Salum Yussuf Ali, wakati alipofanya ziara kwa wafanyabiashara katika baadhi ya maduka mjini Unguja.

Alisema mfumo wa kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki ndiyo unaokubalika kwa mujibu wa sheria za fedha hatua ambayo itawezesha serikali kupata mapato yake.

Alisema kuwa mchakato wa kuanza kwa utaratibu wa kufanya malipo ya kielektroniki kwa majaribio umeonyesha yapo mafanikio makubwa.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara kutoa risiti kwa sababu wapo wanaopuuza katika utoaji wa risiti kitendo ambacho hakikubaliki kwa mujibu wa sheria za kodi na watakaofanya hivyo watalazimika kupigwa faini ya kodi.

"Serikali imeanzisha mfumo wa kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki ikiwamo utoaji wa risiti wakati wa kufanya manunuzi kwa hivyo wafanyabiashara wote wanatakiwa kutoa risiti ambayo ndiyo uhalali wa kufanya biashara na kodi," alisema.

Baadhi ya wafanyabiashara waliotembelewa na maofisa wa Bodi ya Mapato (ZRB), wamefurahishwa na kuwapo kwa mfumo wa kodi wa kielektroniki.

Mfanyabiashara anayemiliki duka la dawa la Fahud Darajani Unguja, ameipongeza bodi ya mapato kwa hatua wanazoichukua ambazo zimelenga kudhibiti upotevu wa mapato ya serikali.

**"Serikali imeanzisha mfumo wa kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki ikiwamo utoaji wa risiti wakati wa kufanya manunuzi kwa hivyo wafanyabiashara wote wanatakiwa kutoa risiti ambayo ndiyo uhalali wa kufanya biashara na kodi," alisema.**

# Hukumu ndogo ya jumuiya JUMAZA kutolewa Feb. 17

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KESI ya Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) dhidi ya Bodi ya Vileo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekwama kwa mara ya pili kutolewa hukumu kutokana na Jaji wa Mahakama Kuu, Abdulhakim Amiri Issa, kuwa likizo ya mwisho wa mwaka.

Akizungumza jana na waandishi wa habari wakili wa JUMAZA, Ruhaiya Kassim Mgeni, alisema Jaji Abdulhakim amepanga Februari 17, mwaka huu, kutoa hukumu dhidi ya pingamizi zilizofunguliwa na mwanasheria kutoka ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali.

"Tulifika mahakamani leo kusikiliza hukumu ndogo ya pingamizi zilizofunguliwa na wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu bahati mbaya kesi imeahirishwa kutokana na kutokamilika," alisema.Katika pingamizi zilizofunguliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanadai kesi ya JUMAZA imefunguliwa kinyume na sheria bila ya kutoa indhari ya siku 60 kabla ya kufungua mashtaka dhidi ya serikali.

Katika kesi ya msingi wanadai Mwanasheria Mkuu na Bodi ya Vileo Zanzibar imetoa vibali kwa kampuni za uingizaji wa pombe zaidi ya tisa badala ya tatu kinyume na kifungu cha 33(1) cha sheria ya vileo namba tisa ya mwaka 2020.

Madai memgine ya JUMAZA, Bodi ya Vileo Zanzibar imeshindwa kusimamia masharti ya baa kuwa umbali mita 1,000 kutoka katika maeneo ya huduma za jamii kama shule, nyumba za ibada, hospitali na makazi ya watu kinyume na sheria kifungu 28(k) cha sheria hiyo.

Aidha, JUMAZA inataka Sheria ya Bodi ya Vileo isimamiwe kama ilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi kabla ya kuanza kutumika Mei 11, mwaka 2020, baada ya kusainiwa na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

Viongozi hao wamekuwa wakifuatilia kesi hiyo, wakiongozwa na Katibu wa Kamati ya Maadili na Taasisi za Kiislamu, Shekhe Abdallah Abasi Mnubi, tangu ilipofunguliwa.

Kesi hiyo imeibua mjadala mkubwa katika jamii kutokana na kuwapo ongezeko la baa karibu na makazi ya huduma za jamii na kuwa kero baada ya nyumba nyingi kugeuzwa kuwa biashara ya vileo na kupigwa muziki nyakati za usiku na kuibua malalamiko kutoka kwa wananchi.




Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui (kushoto), akipokea msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Dola za Kimarekani 114,521.27 kutoka kwa Taasisi ya Helping Hand ya Marekani wakishirikiana na Taasisi ya Muzdalifa iliyoko Zanzibar, Mnazimmoja jijini humo, jana. Kulia ni mshauri msaidizi wa taasisi hiyo, Irfan Khurshid. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# IGP Sirro aagiza kuharakisha ujenzi vituo vya polisi

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, ameagiza kuharakishwa kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa vituo vya polisi vilivyoko Mkokotoni, Mkoa wa Kaskazini pamoja na Kizimkazi Wilaya ya Kusini Unguja, kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi na kupambana na uhalifu.

Sirro alisema hayo alipofanya ziara kuangalia mwenendo wa ujenzi wa miradi ya vituo vya polisi ambao kwa upande wa kituo cha Mkokotoni kimechukua muda mrefu kukamilika.

Alisema ujenzi wa vituo hivyo ni muhimu kwa kuwa vitawawezesha wananchi kuwasilisha malalamiko yao yanayotokana na matukio ikiwamo ya uhalifu na udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema ujenzi unahitajika kwa kiwango kikubwa kwa sababu matukio ya uhalifu ikiwamo udhalilishaji wa kijinsia yameongezeka na kuwa tishio kwa wananchi na wazazi.

Alisema ujenzi wa kituo cha Mkokotoni umechukua muda mrefu kiasi cha kuibua hoja za malalamiko kwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

"Nataka kuona changamoto zilizojitokeza za ucheleweshaji wa kituo cha Polisi Mkokotoni Unguja zinapatiwa ufumbuzi wa haraka na sasa ujenzi wake ukamilike kwa kasi na kuanza kufanya kazi... kitendo cha kuchelewa kukamilika kituo hiki kimetupa wakati mgumu bungeni," alisema.

Aidha, Sirro aliwataka askari wa jeshi hilo kuhakikisha mwaka 2022 unakuwa wa mafanikio kwa jeshi hilo katika kutekeleza malengo yake ya kuwahudumia wananchi na kulinda mali zao.

"Hayo ndiyo malengo ya Jeshi la Polisi kwa mujibu wa Katiba... kulinda na kuweka usalama wa wananchi na kuona mali zao zipo salama," alisema.

Naye Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Muhamad Haji Hassan, alisema utulivu umetawala Zanzibar na Jeshi la Polisi limeongeza kasi ya kupambana na matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia pamoja na dawa za kulevya.

Alisema hivi karibuni serikali imewasilisha sheria mpya ya kuundwa kwa mamlaka ya kupambana na dawa za kulevya na matumaini makubwa ya jeshi hilo ni kufanya kazi na mamlaka hiyo katika kutokomeza dawa za kulevya na Zanzibar kuwa salama.

"Jeshi la Polisi Zanzibar linaendelea na majukumu yake ya kusimamia amani na utulivu pamoja na mali za wananchi ambapo tumeongeza kasi na mikakati ya kupambana na udhalilishaji pamoja na dawa za kulevya," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 13 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**NICHOLAUS RICHARD REUBEN**
**and**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**NEEMA SILAS MAYUNGA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 1 day of 02,2022.

Dated at DAR ES SALAAM this 13 day of JANUARY, 2022.

Registrar/Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PHEBY KAITIBA MURUSURI** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T167 ACY TOYOTA RAV 4** Engine No . **3S2649855** Chassis **No.SXA110222018** Atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Taarifa ya polisi **ARU/ARU/RB/22602/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PANONE & COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T 224 AUC,** chasis namba **FK416J550095** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **KIL/MOS/RB/18068/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FREDRICK MILARD LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 417 AWE – TOYOTA COROLLA.** Chassis namba **AE1140003779.** Engine namba **4A1009069.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **TAN/TAN/RB /590429/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FREDRICK MILARD LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 328 BWG – MITSUBISHI CANTER.** Chassis namba **FE111B555102.** Engine namba **4D305102.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **TAN/TAN/RB /590436/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **YUSUPH AMIRI SHIJA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari lenye namba za usajili **T 813 AKE** injini namba **6D15504213** na chassis namba **FK416K-512661.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/21906/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0768-155793**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ALLEN ALLEN MEMBA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye namba za usajili T 402 BQV,chasis namba SXA110163572, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa DAR/KIJ/RB/21942/2022

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

KAHAMA IMPORT AND EXPORT Atangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC. 491 BLL, yenye Chasiss no; LKXYCJL31E9000071, Engine no; 162FMJEA167335 aina ya SHINERAY XL-150. Yeyote atakeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake Taarifa ya jeshi la polisi: KAH/RB/43/2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## HATI YA KIAPO



Mimi **RAMADHANI MOHAMEDI SAKORO,** mtu mzima mwenye akili timamu, mkazi wa mtaa wa Mapinduzi kata ya Duga, Halmashauri ya Jiji la tanga, bila kushawishiwa na mtu yeyote naapa kama ifuatavyo:-

- KWAMBA, mimi RAMADHANI MOHAMEDI SAKORO ni mmiliki wa Hati ya kiwanja Na. 236 Kitalu Na.29 Ngamiani, Halmashauri ya Jiji la Tanga.
- KWAMBA, Hati Miliki ya kiwanja hicho imepotea na nimefanya juhudi za kutafuta bila mafanikio. Taarifa Polisi, TAN/RB/18497/2022.
- KWAMBA, kwa kiapo hiki naomba Idara ya Ardhi na mipango miji wilaya ya Tanga inipatie hati nyingine ya umiliki wa kianja hicho.

**UTHIBITISHO**
Mimi, RAMADHANI MOHAMEDI SAKORO nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kuanzia aya ya 1-3 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sheria ya viapo
(The Oaths and Statutory Declaration Act.Cap.34 R.E 2002)

**MBELE YA….A.M KHAMISI**
**CHEO…HAKIMU**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LEIMBA OLE KASHUMA**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya GARI(raum) yenye namba za usajili **T 557 DHF** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0674964006**
**MOR /MOR/RB/23045/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MICHAEL B. SUNGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha Chuo chenye namba **BECON 000413** kilichotolewa na CHUO CHA ARDHI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAJ/RB/8393/20.**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Waandamana kupinga utawala kijeshi Sudan

**Khartoum,** SUDAN

MADKTARI wameandamana Sudan na kulaani kushambuliwa na maofisa wa usalama, wakati wa maandamano yanayoendelea mara kwa mara kushinikiza jeshi kurejesha uongozi wa raia, tangu mwaka uliopita.

Jumapili, mwaka huu, madaktari waliandamana kupinga mashambulizi dhidi ya hospitali na vikosi vya usalama.

Pia mashirika ya kiraia yanatoa wito kwa watu kujitokeza tena mitaani, kuandamana dhidi ya utawala wa kijeshi, huku mamlaka ikifuta kibali cha Al Jazeera Mubasher, mojawapo ya vituo vya habari vya Qatar, siku ya Jumamosi, pamoja na vibali vya waandishi wake wawili nchini humo.

Kituo cha habari ambacho kimebobea katika utangazaji wa matukio ya moja kwa moja, kurusha picha za kila aina kuhusiana na maandamano mbalimbali, bila maoni, Al Jazeera Mubasher, kimekuwa kikirusha hewani maandamano ya kupinga mapinduzi katika miezi ya hivi karibuni.

Maandamano ambayo yalikandamizwa vibaya na ambayo yamesababisha mauaji ya watu 64 hadi sasa.

Wizara ya Habari, mwishoni mwa wiki, ilishutumu katika barua ya wazi kile ilichokiita utangazaji usiokuwa wa kitaalamu wa matukio ya Sudan kwenye idhaa ya Al Jazeera.

Ubalozi wa Marekani umeshtumu uamuzi huo wa serikali ya Sudan wa kufuta kibali cha Al Jazeera Mubasher, kinachoiruhusu kufanyia kazi nchini Sudan. **RFI**

## Rais wa Mali aliyepinduliwa madarakani aaga dunia

**Bamako,** MALI

RAIS wa Mali, Ibrahim Boubacar Keita, almaarufu IBK, ambaye alipinduliwa madarakani na jeshi mwaka 2020 amefariki, akiwa na umri wa miaka 76.

Taarifa rasmi imetolewa na mamlaka husika, aliongoza nchi hiyo tangu Septemba, mwaka 2013 hadi Agosti 2020, wakati ambao waasi wa Kiislamu walivamia maeneo makubwa na ghasia za kikabila kupamba moto nchini humo.

Miaka miwili iliyopita aliugua kiharusi, chanzo cha kifo chake mwishoni mwa wiki hakikuwekwa wazi.

Alifariki muda wa saa tatu saa za Uingereza, nyumbani kwake mjini Bamako, mmoja wa ndugu zake alikiambia chombo cha habari cha AFP.

Keita, aliiongoza Mali kwa miaka saba hadi 2020, wakati alipopinduliwa baada ya maandamano makubwa dhidi ya serikali kutokana na jinsi alivyolishughulikia suala la Wanajihad.

Mgogoro wa kiuchumi na uchaguzi ulio huru pia ulisababisha maandamano hayo dhidi ya utawala wake.

Keita alihusika katika siasa kwa zaidi ya miongo mitatu, akihudumu kama Waziri Mkuu kutoka mwaka 1994 hadi 2000.

**REUTERS/BBC**

# Kenya yasajili wapigakura wapya kwa awamu ya pili

**Nairobi,** KENYA

TUME Huru ya kusimamia Uchaguzi nchini Kenya-IEBC, imeanza awamu ya pili ya kuwasajili wapigakura kote nchini humo.

Tume hiyo iliyoshindwa kutimiza malengo ya kuandikisha wapigakura milioni sita kwenye awamu ya kwanza iliyofanya mwaka uliopita inalenga kuandikisha wapigakura milioni 4.5 wakati huu, zoezi hilo litakapokamilika tarehe sita Februari mwaka huu.

Ili kufikia malengo yake kwenye zoezi hili, Tume ya IEBC imesambaza vifaa vya kuwasajili wapigakura katika wadi zote nchini, huku ikilenga kuhakikisha kuwa wapigakura milioni 25 wanashiriki katika upigaji kura, tarehe tisa Agosti mwaka huu.

Tume hiyo ilianza zoezi la kuwaandikisha wapigakura tarehe nne Oktoba hadi tarehe tano Novemba mwaka uliopita, ambapo wapigakura wapya milioni moja nukta tano waliandikishwa. Mwenyekiti wa Tume hiyo Wafula Chebukati amesema kuwa wataruhusu wapigakura wanaotaka kubadilisha vituo vya upigaji kura ama nyaraka zao katika kipindi hiki.

Wapigakura walioko nje ya nchi ya Kenya wataanza kuandikishwa tarehe 21 hadi tarehe sita mwezi Februari, zoezi hilo litakapokamilika. IEBC inalenga kuandikisha wapigakura katika mataifa ya Uingereza, Marekani, Sudan Kusini, Quatar, Falme za Kiarabu na Ujerumani.

Punde tu baada ya zoezi la kujiandikisha litakapokamilika, ukaguzi wa sajili ya wapigakura utafanyika kisha walioandikishwa kuthibitishwa. Ukosefu wa vitambulisho kulisemekana kuchangia uandikishaji mdogo mwaka uliopita. Hata hivyo vijana wametoa sababu tofauti za kutojiandikisha kwa wingi.

Wakenya wanaoishi ughaibuni wangependa kujisajili wameshauriwa kuwasilisha hati zao za usafiri na wawe na umri wa miaka 18 na zaidi kwa ofisa wa usajili.

Hata hivyo Wakenya wanaoishi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki watahitaji kutumia vitambulisho vyao kama ushahidi wa uraia wao kujisajili.

Uchaguzi mkuu uliopita mwaka 2017, watu milioni 15.9 walisajiliwa kupiga kura. Tume ya IEBC tayari imeidhinisha vyama 82 vya siasa kushiriki kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu.

Hata hivyo kinyang'anyiro kikuu kinatarajiwa kuwa kati ya Makamu wa Rais William Ruto wa Chama cha UDA na Raila Odinga ambaye amesema kuwa atawania kwa tiketi ya Muungano wa Azimio la Umoja. **DW**



Mtoa huduma akiweka mwili katika mfuko baada ya mlipuko wa bomu kutokea eneo la Mogadishu, juzi na kuua watu kadhaa, nchini Somalia. **PICHA: REUTERS**

## Uhaba wa mafuta waikumba Uganda

**Kampala,** UGANDA

UGANDA inakabiliwa na uhaba wa mafuta kufuatia foleni ndefu kuwataka wasafirishaji mafuta katika maeneo ya mpakani mwa Malaba na Busia, Mashariki mwa Uganda, kupima Covid-19.

Foleni za malori zinazongoja huduma hiyo zina urefu wa kilomita 70 (maili 43), imeripotiwa.

Madereva wa malori katika eneo hilo, wamekuwa wakiandamana kupinga hitaji la serikali ya Uganda kwamba wapime Covid-19 katika maeneo ya mpakani, bila kujali kama waliwasilisha kipimo cha PCR hasi au la.

Agizo la vipimo mpakani lilitolewa mwanzoni mwa mwezi. Baadaye Uganda ilisitisha lakini tayari kulikuwa na mkusanyiko wa malori katika maeneo ya mpakani.

Uganda, inaagiza mafuta yake yote na bidhaa nyingine za petroli na hutumia takriban lita milioni 6.5 sawa na galoni milioni 1.7 kwa siku.

Bei ya mafuta imekuwa ikipanda kwa kasi tangu mwaka jana, ingawa ongezeko kubwa limeonekana katika wiki iliyopita.

Katika mji mkuu wa Kampala, baadhi ya vituo vya mafuta vimekuwa vikiuza petroli, inayojulikana kama V-power na baadhi ya wasambazaji, ambayo inagharimu shilingi 5,200 za Uganda sawa na dola 1.5 kwa lita moja katika baadhi ya maduka. **BBC**

# SIMBA, YANGA ZAPATA MCHEKEA DROO FA CUP

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF)maarufu Kombe la FA, watakutana na Dar City katika hatua ya 32 ya kinyang'anyiro hicho msimu huu, huku watani zao, Yanga wenyewe wakipangwa kukutana na Mbao FC.

**Katika droo ya michuano hiyo iliyochezeshwa jana inaonyesha mechi ya Simba na Yanga zitakuwa wenyeji wa mechi hizo zitakazoanza kupigwa kati ya Januria 27 hadi 31, mwaka huu.**

Michezo mingine ni Azam FC ambao watawakaribisha Trans Camp katika Uwanja wa Azam Complex huku Biashara United ikiwa nyumbani kupepetana na Mbeya Kwanza, African Lyon dhidi ya Kagera Sugar mchezo utakaopigwa katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

African Sports ya Tanga itawakaribisha Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, KMC FC dhidi ya Ruvu Shooting Uwanja wa Uhuru, Baga Friends yenyewe ikivaana na Catamine FC.

Tanzania Prisons itakuwa mwenyeji wa Rhino Rangers katika Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga, wakati Mbuni FC ya Arusha ikiwakaribisha Lipuli FC na Pamba FC ikivaana na Stand FC ya Mtwara.

Coastal Union ikivaana na Top Boys ya Mkoa wa Ruvuma huku Namungo FC ikiwakaribisha ndugu zao Lindi United katika uwanja wa Ilulu uliopo mkoani humo.

Kwa upande wa Dodoma Jiji FC, itawakaribisha Sumbawanga United katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma huku Polisi Tanzania zivaana na Ndanda FC katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Katika hatua ya 16 bora itakayoanza kuchezwa Februari 22 hadi 27, mwaka huu, mshindi dhidi ya Simba na Dar City atacheza na mshindi kati ya KMC FC na Ruvu Shooting, wakati timu itakayoshinda kati ya Yanga na Mbao FC ikikutana na mshindi dhidi ya Biashara United na Mbeya Kwanza. Mshindi wa mchezo wa Azam FC dhidi ya Trans Camp atacheza na mshindi kati ya Baga na Catamine FC, wakati timu itakayoshinda kati ya Polisi Tanzania na Ndanda akicheza na mshindi dhidi ya Tanzania Prisons dhidi ya Rhino Rangers.

Coastal Union dhidi ya Top Boys itacheza na mshindi kati ya Afrika Sports dhidi ya Mtibwa Sugar huku timu itakayoshinda kati ya Mbuni FC na Lipuli FC ikicheza na mshindi kati ya Dodoma Jiji dhidi ya Sumbawanga.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, mwakilishi wa Yanga ambaye ni Mkurugenzi wa Mashindano wa klabu hiyo, Thabiti Kandoro, alisema wanaziheshimu timu watakazokutana nazo, lakini watahakikisha wanafikia malengo yao.

Alisema Mbao FC ni timu nzuri na wanaenda kukutana nao kwa tahadhari kubwa kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kutwaa mataji mawili ya ubingwa wa ligi na Kombe hilo la Shirikisho.

"Hatutaingia kwa kuwadharau, tutawaheshimu, lakini napenda kuwaambia Mbao FC kuingia kwa tahadhari kubwa kwani tumedhamiria kweli kuhakikisha msimu huu tunatwaa makombe mawili," alisema Kandoro.

Naye Meneja wa Azam FC, Rashid Said, alisema hawana mashaka na kikosi chao kipo tayari kukutana na yeyote kwa sababu wamejipanga kupata matokeo mazuri.

"Kwa sasa tumerejea katika ubora wetu, ukiangalia kiwango tulichokionyesha visiwani Zanzibar kwenye Mapinduzi Cup, itakuwa zaidi katika michezo yetu ijayo," alisema Rashid.




Viungo wa Simba; Pape Sakho akiwa amevalia jezi namba 10 baada ya kuridhia kumwachia Clatous Chama uzi namba 17 aliokuwa akiutumia awali kabla ya kujiunga na RS Berkane ya Morocco. Jezi namba 10 ilikuwa ikitumiwa na Ibrahimu Ajibu ambaye amejiunga na Azam FC. **PICHA: SIMBA**

## DTB FC haikamatiki, Gwambina mkiani

**Na Adam Fungamwango**

MZUNGUKO wa kwanza wa Ligi ya Championship, kutafuta timu tatu zitakazopanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao umemalizika juzi, huku timu mpya ya DTB FC ikiongoza kileleni mwa msimamo kwa kujikusanyia pointi 39, ikiwa pia haijapoteza mechi yoyote mpaka sasa.

Timu hiyo iliyosheheni wachezaji wengi wa zamani waliowahi kuzipitia timu mbalimbali za Ligi Kuu, ikiwamo Simba na Yanga kama vile Mghana Nicolaus Gyan, Mrundi Amissi Tambwe, Juma Abdul na wengineo, inapewa nafasi kubwa ya kuwa ya kwanza kupanda msimu ujao kutokana na matokeo yake kuwa mazuri.

DTB, imecheza mechi 15 za mzunguko wote wa kwanza na kushinda 12 huku ikitoka sare mechi tatu.

Wakati DTB ikiongoza, timu iliyocheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu uliopita na kuteremka, Gwambina, inashika mkia ikiwa haijashinda mechi yoyote mpaka sasa.

Gwambina ambayo ina pointi sita tu mpaka sasa kwa mechi 15 ilizocheza, imezipata kwa kutoka sare mechi hizo sita, huku ikipoteza michezo tisa, ikiwa nafasi ya 16.

Kwenye Ligi hiyo ya Championship, timu nyingine iliyocheza Ligi Kuu msimu uliopita na kuteremka, Ihefu FC, inashika nafasi ya pili kwa kuwa na pointi 35, huku Kitayosce FC ikiwa nafasi ya tatu na pointi zake 28.

Mabingwa wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1990, Pamba FC wako nafasi ya nne kwa pointi 22, huku JKT Tanzania ambayo nayo ilishuka msimu uliopita ikiwa nafasi ya tano kwa pointi 22.

Mwadui FC, timu nyingine iliyoshuka ina pointi 19 nafasi ya 10, Ndanda nafasi ya 13 kwa pointi 19, Mabingwa wa Muungano mwaka 1982, Pan Africans wakiwa nafasi ya 14 kwa pointi 14.

# *Hitimana akunwa kuanza kwa ushindi KMC*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa Uwanja wa Nelson Mandela mkoani Rukwa juzi.

Huo ni ushindi wa kwanza kwa Hitimana tangu alipojiunga na KMC FC, kuchukua mikoba ya John Simkoko na Habib Kondo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema ushindi huo una maana kubwa kwake pamoja na kikosi chake wakati wakipambana kutafuta nafasi ya kusogea nafasi za juu ya msimamo wa ligi hiyo.

Alisema ana ushindi huo hauwezi kumfanya kubweteka kwani bado safari ni ndefu kutokana na timu nyingi kupishana kwa pointi chache.

"Ligi Kuu msimu huu ni ngumu, timu zimepishana pointi chache, ukipoteza unashuka chini ya msimamo kitu hicho hatutaki kitokee, nimeanza vizuri na nitahakikisha tunaendelea kutafuta pointi katika kila mechi iliyopo mbele yetu," alisema Hitimana.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Prisons, Shaaban Kazumba, alisema walihitaji matokeo chanya, lakini kipigo hicho kimeharibu mipango yao, jambo ambalo hawana budi kujipanga kwa mchezo ujao.

"Hatukupaswa kupoteza mchezo huu, tulihitaji matokeo kuliko wapinzani wetu, nawapongeza kwa kupata ushindi na sisi tumeona tulipokosea, sasa tunajipanga kwa michezo ijayo," alisema Kazumba.

## ZISIKUPITE

### DEMBELE KUONDOKA BARCA

WINGA wa Ufaransa na Barcelona, Ousmane Dembele anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo ili kujiunga na Manchester United au Juventus huku Chelsea na Bayern Munich wakiwa wametupwa nje katika harakati za kumsaini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Sport)***

### NAVAS ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inafikiria kuwasilisha ombi la kutaka kumsajili kipa wa klabu ya PSG, Keylor Navas, lakini klabu hiyo ya Ligue 1 inataka kumzuia kipa huyo mwenye umri wa miaka 35 raia wa Costa Rica kutokana na kutokuwa tayari kumuona akiondoka. ***(RMC Sport via Mail)***

### CARLOS KUNG'OLEWA SEVILLA

KLABU ya Newcastle inapiga hatua katika majaribio yao ya kutaka kumsajili beki wa Sevilla na Brazil, Diego Carlos, 28. ***(Express)***

### JUVE YAMTAKA PARTEY

JUVENTUS inamnyatia kiungo wa kati wa Arsenal na raia wa Ghana, Thomas Partey, 28. ***(Sky Sports Italy, via Mail)***

### KARZAWA AWANIWA CHELSEA

CHELSEA ina nia ya kutaka kumsajili beki wa PSG raia wa Ufaransa, Layvin Kurzawa, 29, kwa mkopo, lakini mazungumzo hayajaanza kati yao. ***(Fabrizio Romano on Twitter)***

### BROJA AMULIKWA S'AMPTON

KLABU ya Southampton ipo katika mazungumzo na Chelsea kuhusu uhamisho wa kudumu wa raia wa Alabania ambaye anahudumu katika klabu hiyo kwa mkopo, Armando Broja, 20. ***(Guardian)***

### VLAHOVIC ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imewasilisha ombi la pauni milioni 50 ili kumsajili mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic, 21, huku ikimuuza kiungo wa kati wa Uruguay, Lucas Torreira ili kupunguza gharama ya mchezaji huyo. ***(Metro)***

### DE BEEK AKATAA KWA MKOPO

KIUNGO wa kati wa Manchester United raia wa Uholanzi, Donny van de Beek, 24, amekataa ombi la yeye kujiunga na klabu ya Newcastle kwa mkopo. ***(Telegraph)***

### ARSENAL JICHO KWA SPENCE

KLABU ya Arsenal bado ina hamu ya kumsajili beki wa kulia wa Nottingham Forest aliyepo kwa mkopo, Djed Spence lakini mchezaji huyo wa Middlesborough mwenye umri wa miaka 21, pia anavutiwa na Inter Milan. ***(Mirror)***

### KUONDOKA LEICESTER

KLABU ya Leicester City inajiandaa kumwachia kiungo wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND SASA KUAMUA HATIMA YAKE DORTMUND

**●●● Kwa miezi sita nimeamua kutosema chochote kuiheshimu klabu, lakini sasa mambo yataanza kutokea...**

**DORTMUND,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI Erling Haaland ameziweka katika tahadhari klabu za Ligi Kuu England baada ya kufichua kuwa klabu yake, Borussia Dortmund inamshinikiza kufanya uamuzi kuhusu hatima yake.

Haaland raia wa Norway ambaye kwa muda mrefu amekuwa na lengo la klabu zote mbili za Manchester, Real Madrid na Barcelona amekiri "mambo yataanza kutokea sasa" baada ya Dortmund kumweka wazi kuwa lazima aamue hatima yake.

"Kwa miezi sita nimeamua kutosema chochote kuiheshimu Borussia Dortmund, lakini sasa klabu imeanza kunishinikiza kufanya uamuzi," amesema Haaland mwenye umri wa miaka 21 alipozungumza na shirika la utangazaji, Viasat la Norway baada ya kufunga mabao mawili katika ushindi wa Dortmund wa mabao 5-1 dhidi ya Freiburg kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

"Ninachotaka ni kucheza mpira wa miguu, lakini wao (Dortmund) wananishinikiza kuamua sasa kuhusu hatima yangu, hivyo hiyo ina maana lazima nifanye uamuzi hivi karibuni."

Haaland amefunga mabao 78 katika michezo 77 kwenye mashindano yote akiwa Dortmund tangu alipohamia Bundesliga Januari, 2020 akitokea RB Salzburg.

Kurejea kwake kwa kasi katika ufungaji kumemfanya kuwa mmoja wa nyota wa soka wanaowaniwa zaidi barani Ulaya huku Manchester City, Barcelona, Real Madrid na Manchester United zote zikihusishwa na mshambuliaji huyo wa Dortmund katika miezi 18 iliyopita.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
BRIGHTON
VERSUS
CHELSEA
1 | 4.69
X | 3.64
2 | 1.75

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA: HAKUNA UBINGWA JANUARI



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ameeleza umuhimu wa ushindi wa 1-0 dhidi ya Chelsea pale kwenye Uwanja wa Etihad, lakini akasisitiza kuwa taji la Ligi Kuu England huwezi kushinda Januari.

Kevin De Bruyne alifunga bao lake la tano zikiwa zimesalia dakika 20 kupata ushindi huo dhidi ya mabingwa hao wa Ulaya.

"Ushindi muhimu kwa sababu tunacheza dhidi ya mshindani mkubwa," alisema Guardiola. "Unapopata pointi tatu, hawawezi kupata pointi tatu na ni wiki moja pungufu.

"Lakini Januari hakuna bingwa. Tunaweza kufikiria kuhusu Chelsea, na Liverpool wana mechi mkononi. Wakishinda itakuwa na pointi nane na pointi nane Januari si kitu.

"Nataka kushinda endapo tunastahili, na tulistahili. Ninapenda soka kuwa la haki kwa hiyo, wakati nilikuwa na furaha kushinda dhidi ya Arsenal, hatukustahili. Kushinda wakati unastahili hujisikia vizuri," aliongeza Guardiola.



## Martial ajibu shutuma za Rangnick

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Anthony Martial amepinga kuwa hakukataa kucheza kama kocha wa muda wa klabu hiyo alivyodai kwenye mchezo dhidi ya Aston Villa ambao walitoka sare ya 2-2.


Kocha wa muda wa Man United, Ralf Rangnick alidai kuwa mchezaji Martial hakutaka kujumuishwa kwenye kikosi kilichocheza dhidi ya Aston Villa, baada ya kuwataja wachezaji nane wa akiba na miongoni mwao wakiwapo magolikipa wawili kwenye mchezo wa Jumamosi.

Martial anahitaji kuondoka kwenye dirisha hili la Januari, huku akiwa hajajumuishwa kwenye kikosi tangu Desemba 2, mwaka jana, kwenye mchezo wake wa mwisho ambao Man United walishinda 3-2.

Martial anatumai kuwa dirisha hili atatolewa kwa mkopo ili akapate nafasi ya kucheza mara kwa mara kwenye kikosi cha kwanza, huku timu ya Sevilla ikiwa ndio chaguo la pekee ingawa Barcelona na Juventus nao wanahitaji huduma

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA



# YANGA SC WAFUNGUKA KILICHOIPONZA COASTAL

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Coastal Union juzi, kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Klabu ya Yanga imesema kuwa ilijiandaa kikamilifu kushinda mechi hiyo kwa ajili ya kuvunja mwiko wa wapinzani wao, lakini kuwazima midomo.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli, amesema walikwenda Tanga kwa lengo moja tu, kuhakikisha wanashinda mechi kwa ajili ya kuvunja mwiko, kuzima midomo ya mashabiki wa Coastal Union na kuwahakikishia kuwa msimu huu wana kikosi kizuri chenye uwezo wa kushinda popote pale wanapocheza.

"Kwenye mechi hii wachezaji wa timu zote mbili wamepambana, lakini ni anayejiandaa vizuri ndiye mshindi, na sisi tulijiandaa vizuri zaidi. Tunajiamini na hatuna wasiwasi kwa sababu tuna kikosi kizuri cha kupata ushindi," alisema Bumbuli.

**Alisema maandalizi ya Coastal kwenye mechi yao yalikuwa makubwa mno na ya kushangaza, kitu ambacho hawayafanyi kwenye mechi zingine.**

"Nawaambia hivi Coastal, maandalizi haya waliyoyafanya kwenye mechi hiyo, kuandaa wachezaji, kuunda kamati na mengine mengi, kama wataendelea kufanya hivyo, basi wanaweza kumaliza ligi wakiwa kwenye nafasi ya tatu, lakini kama ikiwa ni tabia yao ya miaka yote mechi yao msimu mzima ni moja tu dhidi ya Yanga tena wakicheza Mkwakwani, basi msimu huu pia watacheza 'play off' kama msimu uliopita," alisema Bumbuli.

Naye nahodha wa Coastal Union, Ntenje Albano, alisema kuwa bao lisilotarajiwa dakika chache kabla ya kwenda mapumziko, ndilo liliwafanya kuwa kwenye wakati mgumu.

"Tulidhani tutakwenda mapumziko tukiwa suluhu, lakini tukafungwa bao lile rahisi, sasa ikawa kazi ya kucheza kwa nguvu ili kurudisha na kufunga lingine, na kwa mechi kubwa dhidi ya Yanga inakuwa mtihani," alisema mchezaji huyo.

Wakati Yanga ikiendelea kujikita kileleni kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 32 kwa mechi 12 ilizocheza, Coastal Union iliyokuwa kwenye nafasi ya tatu, imeporomoka hadi nafasi ya nne kwa pointi zake 17.



Mshambuliaji wa Yanga, Said Ntibazonkiza, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Coastal Union katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## *Mlandege yatema nane, kusajili sita*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mlandege imeweka wazi kuwa tayari imeachana na wachezaji nane katika kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo kinachoendelea visiwani hapa huku ikitarajia kusajili wapya sita.

Mlandege imemaliza mzunguko wa kwanza ikiwa nafasi ya nane katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 24.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Msaidizi wa Klabu ya Mlandege, Salum Mohmed, alisema wachezaji hao walioachwa si kama viwango vyao vimeshuka, bali wamefanya hivyo ili kuwapa fursa ya kupata nafasi zaidi ya kucheza katika timu nyingine.

Alisema wachezaji wote ni wazuri, lakini tatizo ni baadhi yao kutopata nafasi ya kucheza katika kikosi hicho, hivyo wameona ni busara wakawapa fursa ya kwenda kuzitumikia klabu nyingine badala ya kuendelea kusugua benchi.

"Timu yetu wachezaji karibu wote ni wazuri, lakini utakuta baadhi wapo benchi muda mrefu, hawapati namba katika kikosi kulingana na mahesabu ya mwalimu mwenyewe, hivyo tunaona ni busara tukawapa fursa ya kwenda kujiendeleza katika klabu nyingine," alisema.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 18/01/2022


| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1865 | Ben Aknoun vs SC Ain Defla | 1.23 | 5.03 | 11.60 |
| 16:00 | 2199 | Mbeya Kwanza FC vs Azam | 3.37 | 2.74 | 2.28 |
| 17:00 | 5443 | Gaziantep BB vs Yeni Malatyaspor | 1.70 | 3.75 | 4.54 |
| 17:50 | 1345 | AL Jeel vs Al Khaleej Club | 2.94 | 2.94 | 2.38 |
| 18:30 | 1276 | Al Khoor vs Al Rayyan SC | 6.17 | 4.82 | 1.37 |
| 18:30 | 3558 | Umm-Salal SC vs Al Gharafa SC | 2.90 | 3.53 | 2.12 |
| 19:00 | 1869 | Villarreal B vs CD Castellon | 2.04 | 3.24 | 3.33 |
| 19:00 | 2636 | Zimbabwe vs Guinea | 5.34 | 3.36 | 1.71 |
| 19:00 | 3343 | Malawi vs Senegal | 9.70 | 4.36 | 1.36 |
| 19:30 | 5227 | Lazio vs Udinese | 1.61 | 3.89 | 5.12 |
| 20:00 | 1048 | Fatih Karagumruk vs Besiktas | 3.21 | 3.41 | 2.13 |
| 20:00 | 2259 | Konyaspor vs Adana Demirspor | 2.12 | 3.36 | 3.26 |
| 20:00 | 5449 | Lucchese vs Imolese Calcio | 2.07 | 3.23 | 3.62 |
| 20:00 | 5713 | AEK Larnaca vs Paeek | 1.31 | 4.53 | 8.67 |
| 20:30 | 1311 | FC Koln vs Hamburger SV | 1.72 | 3.96 | 4.41 |
| 20:30 | 5847 | 1860 Munich vs Karlsruher SC | 2.94 | 3.44 | 2.33 |
| 21:00 | 3978 | Rayo Majadahonda vs Tudelano | 1.65 | 3.49 | 4.85 |
| 21:00 | 4593 | Harbour View FC vs Molynes | 1.72 | 3.80 | 4.70 |
| 21:00 | 5355 | Mafra vs CF Estrela | 1.87 | 3.26 | 4.09 |
| 22:00 | 1808 | Icasa CE vs Pacajus | 3.52 | 2.75 | 2.21 |
| 22:00 | 3728 | Vitesse Arnhem vs DVS 33 Ermelo | 1.03 | 10.54 | 25.87 |
| 22:00 | 5562 | Betis vs Alaves | 1.49 | 4.28 | 6.37 |
| 22:30 | 1697 | Burnley vs Watford | 2.20 | 3.31 | 3.31 |
| 22:45 | 1087 | Stevenage vs Crawley Town | 2.13 | 3.28 | 3.28 |
| 22:45 | 1227 | Fulham vs Birmingham | 1.23 | 5.68 | 10.77 |
| 22:45 | 1277 | Dundee Utd vs St Mirren | 2.61 | 3.16 | 2.66 |
| 22:45 | 1427 | Livingston vs Dundee FC | 2.18 | 3.15 | 3.35 |
| 22:45 | 1614 | AFC Wimbledon vs Portsmouth | 3.05 | 3.35 | 2.20 |
| 22:45 | 1675 | Sutton United vs Colchester | 1.81 | 3.44 | 4.23 |
| 22:45 | 1819 | Gateshead vs Telford | 1.26 | 5.01 | 9.25 |
| 22:45 | 2228 | VfL Bochum vs Mainz | 3.19 | 3.34 | 2.24 |
| 22:45 | 2377 | Forest Green vs Mansfield | 1.79 | 3.59 | 4.13 |
| 22:45 | 2546 | Preston vs Sheffield Utd | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 22:45 | 2626 | Cambridge Utd vs Doncaster | 1.72 | 3.68 | 4.42 |
| 22:45 | 2854 | Ross County vs Motherwell | 2.45 | 3.15 | 2.86 |
| 22:45 | 3515 | Carlisle vs Hartlepool | 2.34 | 3.19 | 2.95 |
| 22:45 | 3675 | Stockport vs Eastleigh | 1.56 | 4.01 | 5.09 |
| 22:45 | 3999 | Port Vale vs Salford City | 2.14 | 3.24 | 3.29 |
| 22:45 | 4316 | Morecambe vs Wigan | 4.71 | 3.88 | 1.64 |
| 22:45 | 4471 | Rotherham vs Lincoln | 1.47 | 4.34 | 5.92 |
| 22:45 | 5538 | Aberdeen vs Rangers | 5.91 | 4.14 | 1.51 |
| 22:45 | 5569 | St. Pauli vs Borussia Dortmund | 6.59 | 5.19 | 1.40 |
| 22:45 | 5662 | Hearts vs St Johnstone | 1.57 | 3.80 | 5.73 |
| 22:45 | 5915 | Maidenhead U vs Chesterfield | 4.10 | 3.56 | 1.79 |
| 23:00 | 1386 | Brighton vs Chelsea | 4.69 | 3.64 | 1.75 |
| 23:00 | 4866 | Heerenveen vs GO Ahead Eagles | 1.90 | 3.41 | 3.56 |
| 23:00 | 5623 | Juventus vs Sampdoria | 1.44 | 4.49 | 6.41 |
| 23:15 | 1499 | Covilha vs CD Feirense | 2.94 | 3.08 | 2.38 |
| 23:15 | 2904 | Mount Pleasant FC vs Humble Lions FC | 1.43 | 4.05 | 6.56 |
| 23:30 | 2650 | Cadiz CF vs Espanyol | 3.20 | 3.05 | 2.38 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Januari 18, 2022

Nipashe


Haaland kuamua hatima yake UKURASA 21



HAMNIWEZI...

Mabeki wa Mbeya City wakijiandaa kumdhibiti Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya jana na kumalizika kwa 'Wekundu wa Msimbazi' kulala kwa bao 1-0. **PICHA: SIMBA**

## Mukoko aigomea Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga ambayo imemtambulisha mchezaji Chico Ushindi kutoka TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, imesema kiungo wao, Mukoko Tonombe hadi juzi alikuwa bado hajaamua kuondoka, na anaonekana hana furaha kuondoka, badala yake anataka kubaki ili amalizie miezi yake sita ya mkataba iliyobaki.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli amesema kuwa, awali kulikuwa na makubaliano ya kiungo huyo anayemaliza mkataba wa miaka miwili kwenye klabu hiyo kwenda TP Mazembe kwa mkopo wa miezi sita, lakini yeye anaonekana mawazo yake bado anataka kubaki nchini.

"Makubaliano yetu ilikuwa ni kwamba aende TP Mazembe kwa mkopo. Tumempa nafasi hiyo, lakini mwenyewe anaonekana hana furaha ya kuondoka, yeye anataka kubaki Yanga, mpaka juzi ilikuwa hivyo, sisi kwenye mfumo wa usajili tulisharuhusu, lakini naona mwenyewe anaona abaki tu Tanzania, kwa hiyo tunaendelea kusubiri, tupate taarifa kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashindano wa Klabu kabla ya kutoa maamuzi," alisema Bumbuli.

Hata hivyo, alisema kama Tonombe akikataa haina shida kwa sababu klabu hiyo bado kikanuni ina upungufu ya mchezaji mmoja wa kigeni, hivyo haitaathiri usajili wa Chico.

Ofisa habari hiyo pia amepinga kile kinachosemwa na baadhi ya watu kuwa usajili huo ni wa mabadilishano wa wachezaji na TP Mazembe, badala yake kuwa ni usajili wa kawaida tu.

"Hatutabadilishana, ila wao walikuwa na mahitaji ya kiungo, wakataka huduma ya Mukoko na sisi tulihitaji straika baada ya kuumia kwa Yacouba Songne," alisema.

# SIMBA WAGONGWA

**Na Adam Fungamwango**

## ● ● ● Gonjwa la kukosa penalti lazidi kuwa sugu, safari hii lahamia kwa Mugalu, lakini...

HUKU ikikosa mkwaju wa penalti dakika mbili baada ya mapumziko, timu ya Simba imepoteza mechi yake ya kwanza msimu huu baada ya kukubali kupigwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

**'Wekundu wa Msimbazi' hao wamepoteza mechi ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu, baada ya kucheza mechi 10 na kuwaacha watani zao wa jadi, Yanga ambao ndiyo timu pekee iliyosalia haijapoteza mchezo wowote hadi sasa.**

Licha ya Mbeya City kucheza pungufu kwa dakika 47, baada ya mchezaji wake Mpoki Mwakinyuke kuzawadiwa kadi nyekundu kwa kumchezea madhambi Chris Mugalu, waliweza kuizua Simba ambayo kipindi cha pili iliamua kucheza na mastraika wake wote watatu, Mugalu, Meddie Kagere na John Bocco.

Ugonjwa wa Simba ulikuwa ni ule ule wa kukosa penalti, safari hii, Mugalu akiikosesha timu yake kupata angalau sare dakika ya 47, alipogongesha nguzo ya pembeni, uliporejea ulimkuta Bocco akiwa kwenye nafasi nzuri ya kuupiga moja kwa moja, lakini alitaka kuuvuta na kuuweka vizuri, hali iliyompa nafasi kipa Deogratius Munishi 'Dida' kuudaka.

Inakuwa ni penalti ya nne kukosa kati ya tano kwenye Ligi Kuu. Wengine waliokosa ni Bocco kwenye mechi dhidi ya Biashara United, Erasto Nyoni akikosa ilipocheza dhidi ya Ruvu Shooting na Rally Bwalya aliyekosa dhidi ya Azam FC, lakini Bwalya ndiye mchezaji pekee aliyefunga penalti akiipa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania.

Mbeya City ndiyo walianza mechi hiyo kwa kuchangamka zaidi kuliko Simba, kwani dakika ya nne tu Juma Luzio nusura awafunge waajiri wake wa zamani, aliposahauliwa na mabeki wa Simba na kubaki yeye na kipa Aishi Manula, lakini shuti lake la mguu wa kulia lilipaa juu.

Dakika nne baadaye, Samson Madeleke akiwa umbali wa mita zipatazo 35, aliachia kombora kali, lililomlazimu Manula kuruka juu na kuupangua, akiiweka Simba salama.

Ndipo dakika ya 19, straika mkongwe ambaye aliwahi pia kuichezea Yanga, Paul Nonga aliiandika Mbeya City bao, baada ya mpira mrefu uliopigwa nyuma, akawazidi mbio mabeki wa Simba ambao walikosa umakini na kuukwamisha wavuni.

Hadi wakati huo Simba ilikuwa haijafanya shambulio lolote la maana kwenye lango la wenyeji wao. Bao hilo lilionekana kuwazindua wachezaji wa Simba na kujiona sasa wapo uwanjani, wakafanya shambulizi la kwanza dakika ya 23, Bernard Morrison alipoingia ndani ya eneo la hatari na kupiga krosi kwa Mzamiru Yasssin ambaye shuti lake liliwababatiza mabeki wa Mbeya City na kurejea uwanjani.

Mzamiru, nusura afunge bao baada ya kuufuma mpira uliorudishwa na mabeki wa Mbeya City kipa Deogratius Munishi 'Dida' akiwa ametoka golini, lakini waliuwahi na kuufagia kabla haujaingia wavuni.

Kibu Denis ambaye aliwasumbua mno mabeki wa Mbeya City alikosa bao, baada ya kuunganisha mpira wa krosi kutoka kwa Morrison, ukatoka sentimeta chache nje ya lango.

Kipindi cha pili baada ya Mpoki kupewa kadi nyekundu, Mbeya City ililazimika kucheza kwa kuzuia zaidi na kufanya kazi kubwa kuwazuia wachezaji wa Simba waliokuwa wakishambulia mfululizo.

Papara na presha ya wachezaji wa Simba ziliwafanya kukosa mabao dakika ya 58, Sadio Kanoute akipiga shuti nje, huku kichwa alichopiga Bocco dakika ya 70 kiliokolewa kwa ustadi na kipa Dida aliyewahi kuidakia timu hiyo.

Pamoja na mabadiliko ya pande zote, lakini hayakubadili matokeo ya mchezo huo.

Ni matokeo yanayoifanya Simba kuendelea kuwa nafasi ya pili, lakini ikisalia na pointi zile zile 24, saba pungufu ya vinara wa Ligi Kuu, Yanga yenye pointi 32, lakini ikiwa na mechi moja mbele.

Kwa ushindi huo, Mbeya City imepanda hadi kwenye nafasi ya tatu, ikiwa na pointi 19.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >